## BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

# RIPOTI YA KAMATI YA KILIMO, BIASHARA NA UTALII KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

FEBRUARI, 2023

YALIYOMO

SEHEMU YA KWANZA ..... 4

UTANGULIZI ..... 4

SEHEMU YA PILI ..... 6

WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO ..... 6

PROGRAMU KUU ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO ..... 6

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO ..... 7

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU ..... 25

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO. ..... 30

PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KILIMO. ..... 46

WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA ..... 49

PROGRAMU KUU ZA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIAWANDA ..... 50

PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA; ..... 50

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI ..... 53

TAASISI NA MASHIRIKA YALIYOMO NDANI YA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA. ..... 61

1. WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI UNGUJA NA PEMBA ..... 61

2. WAKALA WA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO VIDOGO, VIDOGO NA VYA KATI (SMIDA) ..... 62

3. SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC) ..... 64

WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE ..... 72

PROGRAMU KUU ZA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE ..... 72

PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA

UHIFADHI WA MJI MKONGWE 73
PROGRAMU KUU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI WA UTALII 91
PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YA UTALII 94
SEHEMU YA TATU 97
HITIMISHO 97

KWA MWAKA 2022/2023

## SEHEMU YA KWANZA

### UTANGULIZI

Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii ya Baraza la Wawakilishi imeundwa kwa mujibu wa kifungu cha Kanuni cha 107 cha Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2020 na majukumu yake yametajwa katika Jadweli la kwanza la Kanuni hizo kama ifuatavyo: -

(i) Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia.

(ii) Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa Bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza.

(iii) Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya wananchi ya Wizara husika.

(iv) Kuchunguza na kufatilia Mapato na Matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

(v) Kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Wizara husika ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka.

(vi) Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.

(vii) Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.

(viii) Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika

Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ilianza shughuli zake za kufuatilia utekelezaji wa kazi za maendeleo ya Wizara zifuatazo:-

- Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo;
- Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda; na
- Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale.

Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki nane (8) kwa Unguja Pemba kwa mpango

ufuataao: -

i) Tarehe 21/03/2022 hadi 25/03/2022 kwa upande wa Pemba na kuanzia tarehe 28/03/2022 hadi tarehe 01/04/2022 kwa upande wa Unguja, kwa Wizara zote tatu.

ii) Tarehe 09/08/2022 hadi tarehe 13/08/2022 kwa Pemba na tarehe 16/08/2022 hadi tarehe 20/08/2022 kwa Unguja, kwa Wizara zote tatu.

iii) Tarehe 31/10/2022 hadi tarehe 04/11/2022 kwa Pemba na tarehe 07/11/2022 hadi tarehe 11/11/2022 kwa Unguja.

iv) Tarehe 23/01/2023 hadi 27/01/2023 kwa upande wa Pemba, tarehe 30/01/2023 hadi tarehe 03/02/2023 kwa upande wa Unguja.

Wajumbe wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii wameshiriki kikamilifu katika kazi za Kamati kwa vipindi vyote hivyo, Wajumbe hao ni hawa wafuatao: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mheshimiwa Yussuf Hassan Iddi | Mwenyekiti |
| 2. | Mheshimiwa Aza Januari Joseph | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mheshimiwa Mwanajuma Kassim Makame | Mjumbe |
| 4. | Mheshimiwa Nassor Salim Ali | Mjumbe |
| 5. | Mheshimiwa Saada Ra’dhan Mwendwa | Mjumbe |
| 6. | Mheshimiwa Said Saleh Salim | Mjumbe |
| 7. | Ndugu Mwaka Mwinyi Waziri | Katibu |
| 8. | Ndugu Abubakar Mahmoud Idd | Katibu |

## <u>SEHEMU YA PILI</u>

### WIZARA YA KILIMO UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inaundwa na Idara na taasisi mbali mbali ambazo kwa pamoja zina lenga kutoa huduma kwa wananchi katika kuwaletea maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

## IDARA ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

1. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
2. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
3. Idara ya Kilimo na Uhakika wa Chakula
4. Idara ya Umwagiliaji Maji
5. Idara ya Misitu
6. Idara ya Maendeleo ya Mifugo
7. Idara ya Maendeleo ya Mifugo
8. Afisi ya Afsa Mdhamini –Pemba

## TAASISI ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

1. Taasisi ya Utafiti wa Kilimo
2. Taasisi ya Utafiti wa Mifugo
3. Wakala wa Matrekta na Zana za Kilimo

## PROGRAMU KUU ZA WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO

Katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo inajiendesha kupitia programu kuu tano ambazo ni:

1. Programu Kuu ya Maendeleo ya Kilimo;
2. Programu Kuu ya Maendeleo ya Rasilimali za Misitu;
3. Programu Kuu ya Maendeleo ya Mifugo; na
4. Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Kilimo.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA KILIMO

Programu kuu hii inajumuisha programu ndogo mbili

i) Programu ndogo ya Kuendeleza Miundombinu ya Umwagiliaji Maji na

ii) Programu ndogo ya Maendeleo ya Huduma za Kilimo na Uhakika wa Chakula.

## ZIARA ZA KAMATI KUANGALIA MAENDELEO YA PROGRAMU HII.

Kamati katika kazi zake ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali na kufanikiwa kukagua Miradi ya Maendeleo kwa lengo la kutathmini maendeleo yake pamoja na tija iliyopatikana. Kupitia programu hizi, Kamati ilifanya ziara katika maeneo yafuatayo: -

i) Mradi wa ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Chakula – Dodeani Pemba na Kizimbani kwa Unguja;

ii) Miradi ya Umwagiliaji maji katika Bonde la Mlemele, Kinyasini, Chaani, Machigini, Kibonde Mzungu na Mtwango.

iii) Shamba la kilimo –Tumbe;

iv) Shamba la Kilimo Maungani (MSONGE FARM) na

v) Maabara ya Wadudu – Kizimbani na Machomane Pemba.

## ZIARA KATIKA MRADI WA UJENZI WA GHALA LA KUHIFADHIA CHAKULA (DODEANI) PEMBA

Ujio wa Mradi huu, ulilenga kuondosha kabisa madhara ya Sumu Kuvu nchini, ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliamua kutekeleza miradi ya ujenzi wa maghala 14 kwa Tanzania nzima, kati ya hayo maghala mawili kujengwa Zanzibar, moja kwa upande wa Pemba na moja kwa upande wa Unguja.

Wizara ya kilimo ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania iliingia mkataba wa ujenzi wa ghala Ole Dodeani Pemba na Mkansdarasi World Class Engineering Contractors (W.C.E.C) Ltd tarehe 21.5.2021. Gharama za ujenzi wa ghala hilo ni Ths 872,331,900/-. Ujenzi huu ulitarajiwa kutumia muda wa miezi minane mpaka kukamilika kwake. Aidha, mradi huu unasimaiwa na muhandisi mshauri A.V consult kutoka Dar es Salaam ambapo muhandisi alikabidhiwa eneo la ujenzi huo tarehe 26.11.2021 Na ujenzi ulianza rasmi tarehe 8.6.2021 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 7.2.2022.

Kamati kwa mara nyengine tena ilifanya ziara katika Mradi wa ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Chakula liliopo Dodeani kisiwani Pemba baada ya kutoridhika na maendeleo ya ujenzi wa ghala hilo mwezi Machi mwaka 2022 wakati Kamati ilipokuwa ikiendelea na kazi zake za kawaida za kutembelea miradi iliyopo chini ya Wizara hii ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo.

Kamati ilisikitishwa kuona kwamba Mradi huu bado haujafikia lengo lililokusudiwa.

Kutokana na hali hii, Kamati haijaridhika na hatua iliyofikiwa ya mradi huu kutokana na Mkandarasi wa ujenzi kushindwa kuukamilisha mradi kwa wakati pamoja na kwamba ameshaongezewa muda si chini ya mara tatu.

Kamati ilitoa nafasi kwa Mkandarasi pamoja na Mshauri Elekezi wa mradi, kutoa maelezo ya kina juu ya changamoto zinazokwamisha maendeleo ya mradi huu, ambapo Kamati ilibaini tatizo kubwa la rasilimali fedha kwa Mkandarasi pamoja na Mshauri Elekezi kushindwa kuishauri vyema Serikali, juu ya uwezo mdogo alionao Mkandarasi wa ujenzi wa mradi huu.

Pamoja na maelezo hayo, Kamati pia ilibaini changamoto kadhaa ambazo mradi huu unaendelea kukumbana nazo. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama zifuatazo:

1. Kamati imebaini kuwa Mkandarasi hana wataalamu wa muhimu (key staff) watakaoweza kuukamilisha mradi huu kwa wakati uliopangiwa.

2. Kamati pia imeelezwa kuwa, katika eneo la mradi hakuna vifaa vya ujenzi vya kutosha vya kukamilishia mradi huu, hali inayorudisha nyuma kasi ya maendeleo ya mradi huu. Miongoni mwa vifaa hivyo ni pamoja na matofali, saruji na gypsum powder.

3. Kamati ilibaini kuwa, Mkandarasi hafuati mpango kazi wake kama alivyothibitishwa na Mhandisi Mshauri wa mradi jambo linalomkwaza na kutofikia malengo aliyojipangia kwa wakati.

4. Changamoto nyengine ambayo Kamati iliibaini ni kutozifuata sheria zinazoongoza utekelezaji wa miradi kama hii pale changamoto za utekelezaji zinapojitokeza. Kamati imelibaini hili pale Wizara iliposita kumchukulia hatua za kisheria Mkandarasi wa ujenzi huu mara tu alipoonekena kwamba hawezi kuutekeleza mradi kwa wakati uliopangwa hali iliyopelekea hadi sasa Mradi kusuasua katika utekelezaji wake.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inamtaka Mkandarasi kutafuta wataalamu muhimu na wa kutosha watakaoweza kuukamilisha ujenzi wa mradi huu.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kumsimamia ipasavyo Mkandarasi wa Ujenzi huu na kuhakikisha kuwa anaingiza vifaa vya kutosha na anaufuata mpango kazi wake kwa lengo la kuharakisha ukamilishaji wa ujenzi wa Mradi huu.

3. Kutokana na hali hii, Kamati inaiachia Wizara ya Kilimo jukumu la kumsimamia Mkandarasi wa ujenzi huu ili aweze kuukamlisha mradi kama muda wake wa nyongeza unavyoelekeza. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati, muda alioongezewa Mkandarasi huyu unaishia tarehe 28 Feb. 2023. Kutokana na hali halisi ilivyo, Kamati haina shaka Mkandarasi huyu asiposimamiwa ipasavyo basi hataweza kuukamilisha Mradi huu kwa muda huu uliobakia.

4. Kamati injaishauri Wizara ya Kilimo kukimarisha na kukijengea uwezo kitengo chake cha usimamizi wa miradi ili kiweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo endapo Mkandarasi atashindwa kutekeleza majukumu yake, Kitengo kiweze kumchukulia hatua.

5. Kamati inaishauri Wizara ijiridhishe juu ya uwezo walionao wakandarasi na wasirizike na ***Documents*** zao wanazoziwasilisha.

## MRADI WA UJENZI WA GHALA LA KUHIFADHIA CHAKULA - KIZIMBANI UNGUJA.

Mradi wa Ujenzi wa Ghala la Kuhifadhia Chakula Kizimbani uligharimu jumla ya shilingi za kitanzania Milioni 930,589,050/=, uliochukuwa muda wa miezi minane katika utekelezaji wake, kuanzia tarehe 05/08/2021. Na kwa sasa mradi huu umekamilika. Pamoja na hali hiyo, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA UTEKELEZAJI WA MRADI HUU.

1. Eneo la kuanikia mazao liko wazi, hali inayohatarisha usalama wa mazao yatakayoanikwa uwanjani hapo.

2. Ghala hili liko karibu na makaazi ya watu, ambapo, uwezekano wa kufanyika uharibifu wa mali ni mkubwa katika ghala hilo mara tu litakapoanza kufanya kazi.

3. Hadi Kamati inafika katika Ghala hili, vifaa vinavyohitajika katika matumizi ya ghala na maabara kama Aflatoxin screening kit, Moisture meter, Furmigation sheet, Sand snakes, Weighinig scale, Pallet, Bg closer (Sewing machine), Desktop Computer, UPS, Printer, Ladder na Sampling probe bado havijanunuliwa na kuwekwa katika sehemu husika.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuliwekea uzio eneo lililozunguka Ghala Kizimbani, kwa lengo la kuimarisha usalama wa mazao na kuyanusuru na wadudu pamoja na Wanyama waharibifu watakaoweza kuingia na kuharibu mazao hayo.

2. Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kuishirikisha jamii hiyo katika hatua zote za ujenzi wa ghala hili. Hata hivyo Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuendelea kuishirikisha kikamilifu jamii iliyolizunguka ghala hilo, ili iweze kusaidia katika kuimarisha ulinzi.

3. Kamati inaipongeza Wizara ya Kilimo kwa kumsimamia Mkandarasi wa Ujenzi huu ipasavyo. Hata hivyo, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuendelea kumsimamia Mkandarasi huyu ili kuhakikisha kuwa, marekebisho madogo madogo yaliyobakia yanamalizika kwa wakati uliobakia.

4. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuhakikisha kuwa, vifaa vinavyohitajika katika matumizi ya ghala na maabara, vinanunuliwa kwa wakati

5. Kamati pia inaishauri Wizara ya Kilimo kuhamasisha uzalishaji wa mazao kwa wakulima, ili lengo la kuanzishwa kwa ghala hili liweze kufikiwa.

6. Kamati inaishauri Wizara inapoandaa miradi ifanye Tathmini ya kutosha ili kujua mahitaji stahiki ya mradi huo ili kuepusha kuongezeka kwa gharama wakati wa utekelezaji wa mradi hiyo.

## MAABARA YA WADUDU – KIZIMBANI

Maabara hii ilianzishwa katika mwaka 1984 chini ya ufadhili wa Serikali ya Uholanzi ikishirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Kilimo. Lengo kuu la kuanzaishwa kwa maabara hii ni kuyatambua na kuyatatua matatizo yote yanayoathiri mimea kama vile maradhi, wadudu, na magugu.

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

Katika ziara yake hii, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:

1. Kamati ilielezwa changamoto ya uhaba wa fedha uliopelekea kusita kwa utafiti wa wadudu waharibifu wa tungule(kamtangaze) na inzi waharibifu wa matunda.

2. Upungufu wa wataalamu wa wadudu katika ngazi ya shahada ni changamoto nyengine iliyoelezwa mbele ya Kamati, hali inayorudisha nyuma kasi ya

maendeleo ya kituo hiki.

3. Aidha, Kamati imeelezwa changamoto ya taaluma ndogo walizonazo wafanyakazi kituoni hapo. Wafanyakazi waliowengi hufanya kazi zao kwa kutumia uzoefu zaidi.

4. Ukosefu wa vitendea kazi muhimu katika maabara ni changamoto nyengine iliyoelezwa mbele ya Kamati. Vifaa kama vile komputa, masks, gloves, upatikanaji wake si wa kuridhisha, hali inayopeleka wafanyakazi hao kufanya kazi katika mazingira hatarishi hasa tukizingatia sehemu na mazingira halisi ya kazi zao.

5. Aidha, uchakavu wa majengo ya maabara ya wadudu kunarudisha nyuma mori ya kiutendaji kwa wafanyakazi wa maabara hii.
6. Idadi ndogo ya wafanyakazi katika maabara hii kunazorotesha utekelezaji wa majukumu kituoni hapo, Kamati ilielezwa kuwa ni wafanyakazi tisa tu ndio waliopo kwa sasa.

7. Kamati imebaini changamoto ya dawa za kuulia wadudu, ambapo kwa sasa dawa hizo upatikanaji wake unategemea zaidi wafadhili wa mradi.

8. Katika maabara hii, kuna changamoto kubwa ya ukosefu wa maji, hali inayopelekea usumbufu mkubwa katika utekelezaji wa majukumu kituoni hapo.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na mipango, kuipatia Maabara hii fedha za kutosha kwa ajili ya kuendeshea tafiti zilizopangwa kituoni kwa wakati. Hii itasaidia kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknologia inayoendelea kukua duniani siku hadi siku.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kupeleka maombi ya mahitaji ya wafanyakazi wanaohitajika ndani ya Maabara ya Wadudu Kizimbani katika Wizara ya Utumishi wa Umma ili Maabara iweze kupatiwa wafanyakazi wa kutosha na wenye ujuzi na utaalamu wa wadudu ili lengo la kuanzishwa kwa maabara hii liweze kufikiwa.

3. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, kuwapatia mafunzo wafanyakazi waliopo katika Maabara ya Wadudu Kizimbani kwa lengo la kuwaongezea ujuzi na kuachana na kufanya kazi kwa mazoea.

4. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuwapatia wafanyakazi wa Maabara hii vitendea kazi vya kutosha ili kuziweka salama afya zao hasa tukizingatia mazingira hatarishi wanayokabiliana nayo wakati wa kutekeleza majukumu yao.

5. Kamati inaishauri Wizara kuchukuwa hatua za makusudi katika kuyafanyia ukarabati majengo ya Maabara ya Wadudu Kizimbani. Majengo haya ni muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu na taifa kwa ujumla.

6. Kamati inaipongeza Wizara kupitia Taasisi ya Mifugo kwa ubunifu wake wa kutafuta dawa mbadala ya kudhibiti wadudu waharibifu wa mazao kwa kutumia Kungumanga na karafuu. Kamati inaishauri Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa mifugo, kuendelea kufanya tafiti zaidi juu ya masuala ya wadudu waharibifu wa mazao, ili wakulima wetu waweze kulima kilimo chenye tija.

7. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuharakisha mchakato wa upatikanaji wa maji kwa kuchimba kisima cha uhakika kitakachosaidia katika kutatua changamoto hii muda wote.

### MAABARA YA WADUDU MACHOMANE – PEMBA

Maabara ya Wadudu iliyopo Machomane imeanzishwa rasimn mwaka 1988, ambayo ipo chini ya Kitengo cha Hifadhi na Utibabu wa Mimea Kisiwani Pemba.

Maabara hii imegawika katika sehemu kuu mbili ambazo ni

a) Sehemu ya Uchunguzi wa Wadudu wa Mimea na
b) Sehemu ya Uchunguzi wa Maradhi ya Mimea.

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

Kamati katika ziara yake hii imebaini changamoto zifuatazo:

1. Kamati imebaini upungufu mkubwa wa wataalamu katika Maabara hii. Kamati imesikitishwa sana na idadi ndogo ya wataalamu waliopo katika Maabara hii kwa sasa, hali inayopelekea Maabara kushindwa kufanya kazi zake ipasavyo. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati wafanyakazi waliopo hivi sasa ni wanne tu ambao ni Mkuu wa Maabara, dereva, muhudumu pamoja na mtunza ghala.

2. Changamoto nyengine iliyobainika ni ile ya Maabara hii kutofanya kazi zake ipasavyo, changamoto ambayo sababu yake kubwa ni upungufu mkubwa wa wataalamu pamoja na vifaa na ***reajents*** uliyopo kituoni hapo.

3. Kamati imebaini changamoto nyengine ya kusita kwa shughuli za kitafiti katika Maabara hii. Kamati imeelezwa kwamba, kwa sasa hakuna shughuli nyingi za kitafiti zinayofanyika katika Maabara hii kwa sababu ya ukosefu wa wataalamu, wataalamu waliopo hivi sasa ni wa kufanya shughuli ndogondogo tu.

4. Kamati pia ilibaini changamoto nyengine ya kusuasua kwa zoezi la ukaguzi wa mazao na mimea kwa sababu ya ukosefu wa vifaa vya kufanyia uchunguzi bandarini. Kamati ilielezwa kuwa wafanyakazi waliopo hufanya ukaguzi huo kwa kutumia uzoefu walionao tu, hali inayoweza kupelekea uingiaji wa maradhi ya mimea na mazao kwa urahisi.

5. Aidha, ukaguzi wa mazao na mimea katika viwanja vya ndege na bandarini unakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa maeneo ya kufanyia ukaguzi huo, maeneo yalioyopo hivi sasa ni finyu na si rafiki katika kutekeleza shughuli hizo.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, kushirikiana na Wizara ya Utumishi wa Umma, kutoa ajira za wafanyakazi katika Maabara hii kwa mujibu wa mahitaji yaliyopo ili kuhakikisha kwamba, Maabara hii inafanya kazi muda wote hasa tukizingatia Serikali imetumia fedha nyingi katika kujenga Maabara hii muhimu kwa maendeleo ya wakulima wetu.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, kupeleka wafanyakazi wa kutosha pamoja na vifaa katika maabara hii, kwa lengo la kuihuisha maabara iweze kutekeleza majukumu yake kama sheria inavyoelekeza.

3. Tafiti ndio Shughuli za msingi zinazotakiwa kufanywa katika maabara yoyote ile. Kinyume chake ni maafa na athari kubwa kuenea katika jamii zetu, Hivyo Kamati inaisisitiza Wizara ya Kilimo kupeleka wafanyakazi na vifaa vya kutosha katika Maabara hii, ili lengo la kuanzishwa kwake liweze kufikiwa na tija iweze kuonekena.

4. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuharakisha mchakato wa manunuzi ya vifaa kwa Maabara hii na kuhakikisha ukaguzi wa mazao na mimea katika bandari zetu unafanyika katika hali ya mafanikio kabisa.

5. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo ishirikiane na Wizara ya Mawasiliano, kutenga maeneo yaliyo sahihi yatakayotumika katika kufanya ukaguzi wa mazao na mimea bandarini na katika viwanja vya ndege, kwa lengo la kuepusha uingiaji wa maradhi ya mimea na mazao toka nje ya Zanzibar.

## ZIARA KATIKA MIRADI YA UMWAGILIAJI MAJI - MLEMELE, KINYASINI, CHAANI, MACHIGINI,

Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji maji Mlemele, Chaani na Kinyasini ni miongoni mwa miradi inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo ambayo utekelezaji wake umekuwa ni wa kuridhisha.

## BONDE LA MLEMELE (PEMBA)

Mradi huu ulihusisha ujenzi wa bwawa moja la kuhifadhia maji ya kumwagilia yenye uwezo wa kuhifadhi Lita za ujazo 241,400 za maji, ujenzi wa ploti katika eneo la hekta 44, ujenzi wa mita 7,816 za misingi ya kumwagilia, ujenzi wa misingi ya kutolea maji ya ziada (drainage canals) mita 6,768, ujenzi wa barabara za shambani (farm roads) mita 8653 kwa kiwango cha kifusi na ujenzi wa kiwanja kimoja cha kuanikia mpunga.

Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji Maji katika Bonde hili umegharimu jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 3,882,464.8 sawa na shilingi za kitanzania Bilioni 8,929,669,640.

## BONDE LA KINYASINI (UNGUJA)

Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji katika bonde la Kinyasini unakadiriwa kumwagilia hekta 184 za mashamba yote katika bonde hili.

Jumla ya dola Milioni 150 za Kimarekani zimekadiriwa kutumika katika ujenzi wa miundombinu hiyo chini ya Msahuri wake Elekezi Corea Rural Community. Mradi huu umekamilika kwa asilimia mia moja na takribani wakulima 1,500 wanategemewa kunufaika katika mgao wa mashamba katika eneo hili na hadi Kamati inapokea taarifa hii jumla ya wakulima 1,200 tayari wameshagaiwa maeneo kwa ajili ya kuanza kulima kwa msimu huu wa kilimo.

Kwa upande wa ***Bonde la Umwagiliaji Chaani*** jumla ya hekta 71 za mashamba zitatumiwa na wakulima wa bonde hili ambapo kwa sasa tayari bonde limekamilika kwa asilimia mia moja.

## CHANGAMOTO ZA MIRADI HII KATIKA UTEKELEZAJI WAKE

1. Kuchelewa kwa utekelezaji wa Mradi katika bonde la Umwagiliaji **Mlemele** kulikosababishwa na kutokuwepo kwa zana nzito pamoja na Mshauri Elekezi kutokuwa na wataalamu wa kutosha wa kusimamia kazi hiyo. Changamoto hii ilipelekea kuongezwa kwa muda wa utekelezaji wa Mradi kutoka mwezi Aprili

2022 hadi mwezi Agosti 2022.

2. Changamoto nyengine iliyowasilishwa mbele ya Kamati ni kukosekana kwa bajeti ya kusaidia utatuzi wa baadhi ya changamoto pale zinapojitokeza. Ufafanuzi uliotolewa mbele ya Kamati ulibainisha kwamba, changamoto ya uvunaji wa mifumo ya maji safi na salama ulicheleweshа utekelezaji wa baadhi ya kazi za mradi katika bonde la Umwagiliaji **Mlemele** na kuwakosesha wananchi huduma ya upatikanaji wa maji ya kunywa.

3. Kamati pia ilielezwa changamoto ya kutokuwepo kwa bajeti ya usimamizi na ufuatiliaji katika gharama za utekelezaji wa mradi katika bonde la Umwagiliaji **Mlemele**, jambo lililorudisha nyuma morali ya wasimamizi kwa upande wa Wizara ya Kilimo, kutokana na kutolipwa stahiki zao kwa wakati. (Malipo baada ya saa za kazi)

4. Baadhi ya wananchi walikataa kutoa maeneo yao ili kupisha shughuli za mradi wa bonde la **Mlemele** kufanyika katika kiwango ambacho kinaendana na usanifu wa mradi huo. Changamoto hii ilisababisha kusimama kwa muda utekelezaji wa kazi zilizopangwa na hivyo kupunguza kasi ya utekelezaji kwa mradi huu.

5. Katika bonde la Mlemele, malipo ya fedha za fidia yalichukuwa muda mrefu mbali ya kwamba taratibu zote za malipo zilikuwa tayari zimekamilika. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati, baadhi ya wakulima walishindwa kuwasilisha nambari za akaunti zao za Benki na kupelekea Wizara ya Fedha kupitia Wizara ya Kilimo kushindwa kukamilisha malipo kwa wakulima hao.

6. Changamoto nyengine ambayo imeelezwa Katika bonde la **Mlemele** ni kwamba, wapo baadhi ya wakulima wanaolalamika juu ya mazao yao kuathirika kufuatia ujenzi wa miundombinu lakini hawamo katika orodha ya wakulima waliofanyiwa tathmini.

7. Kukosekana kwa kingo pembezoni mwa madaraja yaliopo katika miradi hii, kunaweza kuhatarisha usalama wa wananchi wanaoishi karibu na wale wanaopita katika maeneo hayo hasa watoto wadogo ambao mara nyingi hupenda kucheza katika sehemu hatarishi kama hizi.

8. Miradi hii yote ipo karibu sana na makaazi ya wananchi. Kamati imewabaini baadhi ya Wananchi katika mabonde hayo (Kinyasini) wakivuna maji, hali inayohatarisha usalama wao. Takataka pia zimeonekana kutupwa pembezoni mwa bwawa la ***Chaani*** ambazo zinaweza kuathiri mandhari nzuri ya mradi huu.

9. Changamoto nyengine ambayo Kamati imeibaini ni uingizwaji wa wanyama katika mabonde haya. Wanyama kama vile ng'ombe walionekana kuenea katika mabonde haya ambao kwa njia moja au nyengine huharibu miundombinu ambayo imejengwa kwa gharama kubwa.

10. Katika bonde la Umwagiliaji Chaani Kamati imebaini changamoto kubwa ya upotevu wa maji ambapo kamati ilielezwa kuwa, kwa sasa mradi umekamilika kwa asilimia zote lakini upotevu huo wa maji utasababisha harakati za umwagiliaji katika mashamba ya wakulima kushindikana.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuweka bajeti maalumu ya kusaidia utatuzi wa baadhi ya changamoto pale zinapojitokeza katika utekelezaji wa miradi kama hii.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kupitia Idara ya Kilimo, kuwashirikisha kikamilifu wananchi wanaoishi karibu na maeneo yanayotarajiwa kuanzishwa miradi mbalimbali ya maendeleo kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati.

3. Hata hivyo Kamati inapongeza juhudi za Wizara za kuwatafuta na kuwaorodhesha wakulima hao kwa lengo la kuwapatia malipo ya fidia zao. Kwa upande wa bonde la Kinyasini Kamati iliarifiwa kuwa wakulima wote tayari wameshalipwa fidia zao na Kamati inachukuwa nafasi hii kuipongeza sana Wizara ya Kilimo kwa hatua hii ambayo imeweza kuondosha kabisa migogoro kati ya wakulima hao na Wizara.

4. Kamati inaishauri Wizara kuharakisha zoezi la kuwapatia stahiki zao wakulima walioathirika kufuatia ujenzi wa miundombinu katika bonde hili la Mlemele, lengo ni kuepusha migogoro kati yao na Wizara.

5. Kwa kuzingatia usalama wa wananchi wanaoishi karibu na miundombiunu ya Umwagiliaji maji, Kamati inaishauri Wizara kulichukulia umuhimu wa aina yake suala la kujenga uzio katika maeneo yote ya miradi pamoja na kuimarisha ulinzi katika maeneo hayo. Aidha, ujenzi huo wa uzio utasaidia sana kuzuia uharibifu wa mazingira unaofanywa na wananchi hao.

6. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Kamati za Ulinzi na usalama za Mikoa na Wilaya katika kulitafutia ufumbuzi wa kudumu suala la uingizwaji wa wanyama katika mabonde ya Umwagiliaji kwa lengo la kuzuia uharibu wa miundombinu ambayo imejengwa kwa gharama kubwa.

7. Mitaro katika mabonde ya Umwagiliaji maji (***Kinyasini na Chaani*** imepita karibu sana na makaazi ya watu, Kutokana na hali hii Kamati inaishauri Wizara kupitia Idara ya Kilimo kuwapatia wananchi hawa elimu ya kutosha juu ya kuitunza mitaro hii muhimu kwa wakulima wetu na taifa kwa ujumla. Uwepo wa miundombinu hii ni hatua moja kubwa ya maendeleo katika sekta ya kilimo nchini.

8. Kutokana na hali ya upotevu wa maji katika bonde la Chaani, Kamati inaishauri Wizara kupitia Idara ya Kilimo kuchukuwa hatua za haraka za kuirekebisha hali hii, ili mradi huu uweze kuwanufaisha wananchi wa maeneo husika.

9. Kwa ujumla Kamati haikuridhika kwa baadhi ya utekelezaji wa miradi hii ya Umwagiliaji hasa tukizingatia fedha nyingi zimetumika tumika na miradi imekamilika lakini tija yake haijaonekana. Hivyo Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo isimamie kwa karibu sana miradi kama hii pale inapofika katika jamii ili thamani ya fedha halisi iweze kuonekana.

## BONDE LA UMWAGILIAJI MACHIGINI - PEMBA

Ni miongoni mwa mabonde matatu ya umwagiliaji yaliyomo katika Wilaya ya Mkoani. Bonde hili lina ukubwa wa ekari 62.5 sawa na hekta 25 zinazotumika kwa kilimo cha mpunga.

Ujenzi wa miundombinu ya Umwagiliaji katika bonde hili ulifanyika katika awamu tatu tofauti, ukihusisha ujenzi wa banio, ukataji wa ploti, uwekaji sawa wa mashamba, uchimbaji wa misingi ya udongo ya kumwagilia, uchimbaji wa kisima, uimarishaji wa matuta na ujenzi wa misingi ya kumwagilia kwa saruji. Kazi zote hizi zilifanyika chini ya usimamizi wa miradi tofauti ya maendeleo ikiwemo FAO, SMZ, TASAF na GSFP, miradi ambayo ilichangia kwa kiasi kikubwa katika upatikanaji wa fedha zilizosaidia kukamilika kwa shughuli hizi.

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA BONDE LA UMWAGILIAJI - MACHIGINI.

Kamati katika ziara yake hii, ilibaini changamoto kadhaa ambazo kwa kiasi kikubwa zinazorotesha juhudi za wakulima wa bonde hili za kujiletea maendeleo endelevu katika sekta hii ya kilimo. Miongoni mwa **changamoto** hizo ni kama hizi zifuatazo:

1. Kamati imebaini kuwepo kwa madeni ya umeme ya muda mrefu kituoni hapo, madeni ambayo yanarudisha nyuma kasi ya maendeleo ya wakulima, ambapo upatikanaji wa huduma hii muhimu katika kuendeleza shughuli za umwagiliaji katika bonde hili imekuwa ni changamoto. Kwa mujibu wa taarifa iliyopokelewa mbele ya Kamati, karibu shilingi Milioni mbili na laki tano zinadaiwa na Shirika la Umeme Zanzibar.

2. Kupanda na kushuka kwa huduma ya umeme kituoni hapo kunaathiri upatikanaji wa maji ya kumwagilia katika mashamba ya wakulima katika bonde hili, hali inayowarudisha nyuma wakulima kuweza kuchangia huduma hii kwa wakati unaostahiki.

3. Uharibifu wa miundombinu ya umwagiliaji unaofanywa na wananchi unawaathiri sana wakulima katika bonde hili. Wafugaji wanaonekana kuingiza mifugo yao ndani ya mashamba ya wakulima na kuharibu miundombinu iliyojengwa kwa gharama kubwa.

4. Kamati pia ilielezwa changamoto ya kutolipwa kwa fidia kwa baadhi ya wananchi waliopitiwa na miradi katika bonde hili. Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa mbele ya Kamati, karibu shilingi Milioni 12 zinadaiwa na wananchi hao.

5. Utaratibu usioridhisha wa ujenzi wa mitaro ya kumwagilia maji katika mashamba ya wakulima ni changamoto nyengine iliyobainika katika bonde hili. Wakulima walisikika wakilalamika kuwa, upotevu wa maji unaleta usumbufu mkubwa katika harakati nzima za umwagiliaji katika mashamba yao, hasa pale maji hayo yanaposhindwa kufika katika mashamba hayo kama inavyotakiwa na hatimae lengo la kuwepo kwa mradi huu linashindwa kufikiwa.

6. Kamati imebaini kuwa, ujenzi wa miundombinu ya bonde hili la umwagiliaji umetumia gharama kubwa lakini hadi leo tija haijapatikana.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya Umwagiliaji, kuharakisha malipo ya madeni ya umeme yanayodaiwa na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) ili kutoa fursa ya upatikanaji wa huduma hii muhimu katika bonde hili, iweze kuwa ya uhakika na ya muda wote.

2. Kamati inaishauri Wizara kupitia Idara ya Kilimo kutafuta nishati mbadala kwa ajili ya upatikanaji wa maji katika mabonde hayo kwavile gharama za umeme ni kubwa na wakulima wanashindwa kugharamia gharama hizo.

3. Kufuatia uharibifu wa miundombinu ya umwagiliaji katika bonde hili, Kamati inawashauri wakulima kushirikiana na Idara ya Kilimo kuhakikisha kuwa wanawadhibiti wote wanaohusika na uharibifu huu, kwa kuwachukulia hatua zinazostahiki pale wanapowabaini kufanya uharibifu huo. Aidha Kamati inashauri kuundwa kwa Kamati za ulinzi za Wilaya na Mikoa zitakazosaidia kuimarisha ulinzi katika mashamba haya.

4. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Idara ya Kilimo kufuatilia kwa karibu miradi hii ya Umwagiliaji wakati wa utekelezaji wake, ili kuepusha changamoto ambazo zinaweza kukwamisha malengo ya kuwepo kwa miradi hii. Aidha, elimu zaidi iendelee kutolewa kwa wakulima hawa juu ya kuzitatua changamoto zinazowakabili katika kuendeleza kilimo chao.

5. Kamati haikuridhika na utekelezaji wa mradi Machigini, hivyo tunashauri Wizara iwe na utaratibu wa kufanya tathmini na kujirisha kabla ya kupokea miradi kutoka kwa Mkandarasi, lengo ni kuona miradi hii inaleta tija na kuhakikisha kwamba,

thamani halisi ya fedha iliyotumika inaendana na uhalisia wa miradi yenyewe.

## BONDE LA UMWAGILIAJI - KIBONDE MZUNGU NA MTWANGO

Ni Miongoni mwa Mabonde ya Umwagiliaji ambayo wakulima wa maeneo hayo wanajighulisha na kilimo cha mpunga cha umwagiliaji maji.

Bonde la Umwagliaji Kibonde Mzungu lina ukubwa wa Hekta 22, ambapo wakulima 193 wanalitumia bonde hili kwa shughuli za kiimo hicho. Bonde la Umwagiliaj Mtwango lina ukubwa wa Hekta 83.6.

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

Kamati katika ziara yake hii imebaini changamoto zifuatazo:

1. Uhaba mkubwa wa pembejeo za kilimo ikiwa ni pamoja na mbolea unaowakabili wakulima wa mabonde haya ni changamoto iliyoelezwa mbele ya Kamati.

2. Changamoto nyengine iliyobainika ni ile ya uingizwaji wa wanyama katika mabonde haya. Wakulima walisikika wakilalamika juu ya uharibifu mkubwa wa miundombinu ya Umwagiliaji katika mashamba yao unaofanywa na Wanyama hao.

3. Kamati pia imebaini tatizo la maji kushindwa kufika katika mashamba ya wakulima kutokana na kukosa ubora na viwango kwa miundombinu pamoja na vifaa zikiwemo bomba za maji, ambazo zinaonekana kuchakaa sana, jambo linalorudisha nyuma maendeleo ya kilimo hiki katika mabonde hayo. Kutokana na hali hii, kamati haikuridhika na utekelezaji wa mradi huu.

4. Aidha, malipo ya huduma ya maji ya kumwagilia katika mashamba ya wakulima

ni changamoto nyengine iliyoelezwa mbele ya Kamati. Wakulima waliopo hali zao ni duni wanashindwa kugharamia huduma hiyo.

5. Barabara ya kuingilia katika mashamba ya wakulima ni changamoto nyengine iliyobainika, Kamati imeshuhudia kwa macho yake uchakavu wa barabara hiyo hali inayokwamisha maendeleo ya kilimo hasa siku za msimu wa mvua kubwa, pale wakulima wanaposhindwa kusafirisha mazao yao toka mashmbani.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Serikali kuu kufanya utaratibu wa kuwapatia wakulima wa mabonde haya, pembejeo za kilimo ikiwa ni pamoja na mbolea japo kwa kupitia mikopo, ili waweze kuimarisha kilimo chao. Kwa sasa, bei za pembejeo hizi ni kubwa na wakulima wanashindwa kuhimili.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kushirikiana na Vikosi vya ulinzi na Usalama vya Mikoa na Wilaya ambavyo vitaweza kusaidia katika kuimarisha ulinzi katika mabonde yote. Aidha, jumuiya ziliopo katika mashamba haya ziandae kanuni ndogondogo zitakazotoa miongozo ya adhabu kwa wale wote watakaobainika kuingiza mifugo katika mashamba ya wakulima. Kamati inaamini kwamba kuwepo kwa vikosi pamoja na kanuni ndogondogo, kutasaidia sana katika kuliondoa tatizo hili hasa tukizingatia kwamba, wafugaji hawa ni miongoni mwa wakulima wenyewe.

3. Kamati ilielezwa kuwa, kuboreshwa kwa misingi ya asili ya kuingizia maji katika mashamba haya ndio suluhisho la suala hili. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuimarisha Miundombinu ya maji itakayorahisisha uingiaji wa maji katika mashamba ya wakulima, ili kilimo hiki kiweze kuleta tija kwa wakulima na taifa kwa ujumla.

4. Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, kupitia wataalamu wake wa ujenzi wa

miundombinu ya umwagiliaji, kushirikiana kikamilifu na wakulima muda wote katika kuona kwamba, miundombinu inayojengwa inaleta tija katika kilimo chao. Vilevile wataalamu hao wawe karibu sana na wakulima katika kuwapatia elimu na miongozo sahihi pale zinapotokea changamoto katika harakati zao hizi. Kufanikiwa kwa suala hili kutawawezesha wakulima hawa kulima kilimo chenye manufaa kwao na taifa kwa ujumla.

5. Kamati inaishauri Wizara kupitia Idara ya Kilimo kutafuta nishati mbadala ya upatikanaji wa maji katika kumwagilia mashamba ya wakulima kwavile gharama za umeme ni kubwa na wakulima wanashindwa kugharamia gharama hizo.

6. Kutokana na uchakavu mkunbwa wa miundombinu ya barabara ya kuingilia katika mashamba ya wakulima, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kushirikiana na Wizara ya Miundombinu kuifanyia matengenezo barabara hiyo, ili kuwaondolea wakulima usumbufu wanaoendelea kuupata hivi sasa.

7. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuharakisha ujenzi wa ofisi katika mabonde yote ili kuwatatulia changamoto ndogondogo zinazowakabili wakulima hao.

## SHAMBA LA KILIMO -TUMBE

Shamba la Kilimo liliopo Chwaka -Tumbe lina ukubwa wa hekta 29.2 kwa sasa, na lenye minazi 531.

## CHAMNGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

Katika ziara yake hii, Kamati ilielezwa changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na:

1. Wizi wa mazao uliokithiri unarudisha nyuma juhudi za kulihudumia shamba hili. Wananchi waliolizunguka eneo la shamba hili, huingia shambani na kuiba

rasilimali ziliomo shambani humo, ikiwa ni pamoja na nazi.

2. Eneo la shamba hili ni kubwa lakini kamati imebaini kuwa bado Wizara haijachukuwa hatua madhubuti za kuliendeleza shamba hili.

3. Kamati imebaini changamoto ya shamba kuwa wazi (kukosa uzio) kunakotoa fursa kwa watu wasio waaminifu kuingia katika shamba na kufanya uharibifu.

4. Ukosefu wa ofisi kwa wafanyakazi wa shamba hili ni changamoto nyengine ambayo kamati iliibani. Kibanda kidogo kisicho rafiki hata kidogo ndio kinachotumika kama ofisi kwa sasa.

5. Uhaba mkubwa wa wafanyakazi katika shamba hili ni changamoto nyengine iliyobainika. Ni wafanyakazi 7 tu (wanaume watano na wanawake wawili) ndio waliopo katika shamba hili, ambao wanashindwa kutekeleza majukumu ipaasavyo.

6. Mashirikiano madogo yaliopo kati ya wananchi (wakulima) waliopewa maeneo ya kilimo katika shamba hili na Idara ya Kilimo ni changamto nyengine iliyoelezwa mbele ya Kamati.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuimarisha ulinzi katika shamba la Kilimo Tumbe kwa kuishirikisha kikamilifu jamii iliyolizunguka shamba hili, lengo ni kuzuia uharibifu na wizi unaendelea siku hadi siku.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuandaa mpango kazi utakaosaidia katika kuliendeleza shamba hili, ili kusudi lengo la kuwepo kwake liweze kufikiwa.

3. Katika kufanikisha suala la kuzuia uharibifu katika shamba hili, Kamati inaishauri Wizara kujenga uzio japo kwa kutumia waya kwa hatua za awali.

4. Kamati inaishauri Wizara kuchukuwa hatua za makusudi kuhakikisha wafanyakazi katika shamba la Kilimo Tumbe, wanajengewa mazingira bora ya kiutendaji kwa kuwajengea ofisi ya kisasa, itakayokidhi huduma zote muhimu za kibinaadamu ikiwa ni pamoja na maliwato.

5. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Utumishi wa Umma, kuongeza idadi ya wafanyakazi katika shamba hili kwa lengo la kuongeza kasi na tija katika maendeleo ya kilimo nchini. Aidha, Kamati inawapongeza wafanyakazi wachache waliopo kituoni hapo, kwa kuweza kutekeleza majukumu yao ipasavyo.
6. Kupitia hali hii, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Idara ya Kilimo kuendelea kuwaelimsha (wananchi) wakulima juu ya fursa waliyopewa na faida zake.

## MSONGE FERM (MAUNGANI)

Kamati ilipata fursa ya kutembelea katika taasisi hii ambayo ni muhimu sana kwa maendeleo ya taifa letu kutokana na umuhimu wake.

Ni miongoni mwa wadau wakubwa wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo.Taasisi hii ipo chini ya Mkurugenzi Mwatima Abdalla Juma ambayo, ilianzishwa mwaka 2016 kwa lengo la kutoa elimu juu ya kilimo hai na endelevu. Katika kulifanikisha hili taasisi hii inatoa elimu kwa kuzingatia programu za muda mrefu na muda mfupi zinazojumuisha mafunzo ya nadharia na vitendo ambapo vijana kuanzia umri wa miaka 18 hadi 23 wanapokelewa kujiunga na mafunzo hayo bila ya kuzingatia vigezo vikubwa vya elimu.

- Kamati inaipongeza sana taasisi hii kwa juhudi zake ilizozichukuwa na jinsi ilivyojitoa katika kuwasaidia vijana juu ya masuala mbalimbali yanayohusu kilimo hai, wakiwa na lengo la kuwakomboa vijana hawa kuondokana na tatizo la ajira.

- Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya kilimo kuwa na program maalumu wa kukiendeleza kilimo hai kutokana na umuhimu wake kwa sasa, ambacho ni kilimo chenye manufaa kwa afya zetu, mazingira yetu, utalii wetu na hata kwa

soko la bidhaa zetu.

- Aidha Kamati inaipongeza Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa mashirikiano yake mazuri injayoendelea kuyatoa kwa Taasisi zake binafsi katika kuimarisha kilimo nchini.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA RASILIMALI ZA MISITU

Programu kuu hii inatekelezwa kupitia programu ndogo ya Uhifadhi na Maendeleo ya Misitu.

## ZIARA ZA KAMATI KUANGALIA MAENDELEO YA PROGRAMU HII.

i) Msitu wa Hifadhi Mtambwe Kusini na Kaskazini – Pemba na

ii) Msitu wa Hifadhi Masingini - Unguja;

## ZIARA KATIKA MSITU WA HIFADHI MTAMBWE KUSINI NA KASKAZINI, (PEMBA) NA MASINGINI KWA UNGUJA.

**Msitu wa Jamii Mtambwe** una jumla ya hekta 2,049.24 kati ya hizo hekta 282.5 ni kwa Msitu wa Mtambwe Kaskazini na hekta 1777.5 kwa Msitu wa Mtambwe Kusini.

Hii ni miongoni mwa misitu ya jamii ambayo Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo chini ya usimamizi wa Idara ya Misitu Pemba ina lengo la kuipandisha hadhi Misitu hii kwa dhamira ile ile ya kuinusuru na uharibifu unaoendelea kufanyika siku hadi siku katika misitu hii.

Mchakato wa upandishaji hadhi Misitu hii, ulianza mnamo mwaka 2020 kwa mashirikiano baina ya Idara ya Misitu na jamii ya Mtambwe Kusini na Kaskazini, ambazo ndizo jamii zinazozunguka Misitu hii.

**Msitu wa Hifadhi wa Maumbile Masingini** ni miongoni mwa Misitu ya Hifadhi ya Serikali, ambayo ilianzishwa tangu mwaka 1955 na Serikali ya kikoloni kwa tamko la Government Notice No.31 na kuutangaza Msitu huu kuwa Msitu wa hakiba (Forest Reserve).

Kwa mujibu wa takwimu za mwaka 1996 kupitia Sheria ya Usimamizi na Uhifadhi wa Misitu nambari 10, hifadhi ya Msitu huu ilitambuliwa na kubainisha jumla ya hekta 566 zilizouzunguka msitu huu, Msitu ambao ulipandishwa hadhi rasmin na kuwa Msitu wa

Hifadhi mwaka 2004.

CHANGAMOTO ZOLIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HIZI

1. Kamati ilibaini changamoto ya uharibifu wa Misitu hii, unaoendelea kufanywa na wananchi wanaoishi karibu na misitu kwa matumizi mbalimbali ya kijamii ikiwa ni pamoja na kukata kuni, kupasua mbao na kupiga tanu za mkaa, hali inayoathiri na kupelekea upotevu wa miti mikubwa ya asili iliyomo ndani yake.

2. Changamoto nyengine ambayo imeelezwa mbele ya Kamati ni ile ya matumizi ya misumeno ya moto kinyume na sheria na taratibu zilizowekwa na Serikali kwa kuihujumu miti mikubwa iliyomo katika msitu wa Mtambwe Kusini na Kaskazini. Kamati imesikitishwa sana kuona taasisi muhimu zilizowekwa katika masuala ya ulinzi wa mali za jamii, ndizo zilizo mstari wa mbele katika matumizi ya misumeno hii, ambayo ni muda mrefu sasa Serikali imepiga marufuku matumizi yake kutokana na athari zake kubwa katika jamii.

3. Aidha, viongozi wa Shehia kuwa na mamlaka ya juu kuliko jamii iliyozunguka misitu ya Mtambwe, katika suala zima la kuharibu mazingira kumeonekana kuathiri sana shughuli za kiutendaji katika kuiendeleza misitu hii. Kamati ilielezwa kuwa viongozi hawa hukiuka mipaka yao ya kiutendaji hali inayoathiri sana utekelezaji wa majukumu katika kuiendeleza misitu hii muhimu nchini.

4. Kamati imebaini ukosefu wa uzio katika maeneo yote yaliyozunguka misitu hii, hali inayotoa fusra kwa wananchi kuendelea kuivamia misitu na kuendeleza hujuma siku hadi siku.

5. Motisha mdogo kwa wafanyakazi waliopo katika misitu ni changanmoto nyengine ambayo ilielezwa mbele ya Kamati, hali inayorudisha nyuma hamu ya kiutendaji. Kutokana na hali hii, Kamati inaishauri Wizara pale zinapotokezea fursa za mafunzo, wafanyakazi hawa nao wapatiwe mafunzo hayo kwa lengo la kuwaongezea uelewa pamoja na ari ya kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

6. Ulinzi usio wa kuridhisha katika maeneo yote ya misitu ni changamoto inayochangia kwa kiasi kikubwa katika uharibifu wa misitu hii. Kamati imebaini

kuwa walinzi waliopo katika misitu hii ni wachache ambao hawawezi kukidhi haja iliyopo hasa tukizingatia ukubwa wa maeneo haya. Aidha, imeelezwa kuwa, Walinzi waliopo wanakosa vifaa vya ulinzi kama vile silaha ambazo wangeweza kuzitumia katika kukabiliana na wahalifu na waharibifu wa misitu hii.

7. Idara ya Misitu imeonekana kuwa nyuma sana kiutendaji, hali inayopelekea kuwepo kwa malalamiko mengi juu ya uharibifu wa misitu yetu.

8. Changamoto ya usafiri ni changamoto nyengine iliyobainika. Idara ya Misitu hushindwa kutatua kesi za papo kwa papo hasa kesi za wizi na uharibifu wa misitu hii pale zinapotokezea.

9. Katika msitu wa Masingini, miundombinu ya barabara iendayo katika msitu huo haiko rafiki hasa kwa wageni kuweza kufika huko kwa urahisi, Kwa mujibu wa taarifa iliyopokelewa mbele ya Kamati ni kwamba, wageni wanapoteza hamu ya kufika katika msitu huu, kwa sababu ya miundombinu yake kuwa mibovu.

10. Wafanayakazi katika msitu wa hifadhi Masingini walisikika wakielezea changamoto kubwa ya ukosefu wa vitendea kazi unaowakabili katika utekelezaji wa majukumu yao. Miongoni mwa vitendea kazi hivyo ni pamoja na Rain boots, Rain caot, mabero na reki.

11. Uchakavu wa jengo linalotumika kama ofisi katika Msitu wa Masingini, unaondosha taswira nzuri iliyopo katika ofisi hiyo.

12. Kamati imebaini changamoto ya kuchelewa kwa matumizi ya mfumo wa kielekroniki katika kukusanya mapato katika msitu wa Masingini.

13. Changamoto nyengine ambayo Kamati iliibaini ni ile ya uchakavu na ubovu wa Mnara ambao ulikuwa ukitumika katika kuangalia muonekano wa kisiwa cha Zanzibar, mnara ambao kwa sasa uko hatarini kuanguka. Malighafi iliyotumika

kutenegenezea mnara huu, inaonekana kuathiriwa na wadudu hali inayohatarisha uwepo wake.

14. Changamoto ya ushirikiano mdogo baina ya jeshi la Polisi na Idara ya misitu pale wanapowapeleka wahalifu ambao wanahujumu misitu.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaipongeza Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya Kilimo kwa maamuzi yake sahihi ya kutaka kuanzisha kikosi cha ulinzi (Jeshi Ussu), kikosi ambacho kitasaidia sana katika kuimarisha ulinzi katika misitu yetu. Aidha, Kamati inaishuari Wizara ya Kilimo kuharakisha mchakato wa uanzishwaji wa kikosi hiki kwa lengo la kuboresha suala la ulinzi katika misitu yote iliyopo nchini. Kufanikiwa kwa uanzishwaji wa kikosi, hiki kutasaidia sana katika uhifadhi wa misitu kuepukana na uharibifu na uvamizi unaoendelea kufanyika siku hadi siku.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya Misitu Pemba, kuliangalia kwa umakini mkubwa suala la matumizi ya misumeno ya moto, ambayo inaonekana kutumiwa na watu wachache wasioitakia mema nchi yetu, na hatua za kisheria zichukuliwe kwa wale wote watakaokiuka maagizo ya Serikali juu ya matumizi ya kifaa hiki. Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya Misitu kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya athari mbaya kwa matumizi ya kifaa hiki.

3. Kamati inaishauri Wizara kupitia Idara ya Misitu Pemba, kuendelea kushirikiana kikamilifu na viongozi wa shehia zilizozunguka misitu ya Mtambwe Kusini na Kaskazini katika suala zima la kutekeleza majukumu katika kuilinda na kuhifadhi misitu kwa maslahi ya taifa zima.

4. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuyahifadhi maeneo yote yaliyozunguka misitu ya hifadhi nchini kwa kuyajengea uzio ili kuyanusuru na uvamizi unaoendelea kufanywa na wananchi wanaoishi karibu na maeneo hayo.

5. Kamati inaishauri Wizara pale zinapotokezea fursa za mafunzo, wafanyakazi wa Idara ya Misitu wapatiwe mafunzo hayo kwa lengo la kuwaongezea uelewa pamoja na ari ya kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

6. Kamati inaishauri Idara ya Misitu kushuka kwa jamii, kwa lengo la kuwapatia elimu na miongozo sahihi katika kuiendeleza na kuiimarisha misitu iliyopo nchini ili kuzuia kabisa uharibifu unaoendelea kufanyika na malengo ya kuwepo kwake yaweze kufikiwa.

7. Kamati inaishauri Wizara kuipatia Idara hii usafiri wa uhakika kwa lengo la kuwawezesha kuzitatua kesi za uharibifu na wizi wa misitu kwa wakati muafaka.

8. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kushirikiana na Wizara ya Miundombinu, kuifanyia matengenezo barabara iendayo katika msitu wa Masingini, ili wageni wenye nia ya kufika kituoni hapo, waweze kufika kwa urahisi na bila ya usumbufu wa aina yoyote.

9. Katika kuhakikisha kuwa wafanyakazi katika Mistu yote ya hifadhi wanafanyakazi katika mazingira bora na salama, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, kununua vifaa vyote vinavyohitajika na kuwapatia wafanyakazi hawa kwa lengo la kuwakinga na maafa wakati wa kutekeleza majukumu ya kila siku hasa pale wanapoingia msituni kwa ukaguzi na shughuli nyengine.

10. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kulifanyia ukarabati jengo la Ofisi katika Msitu a Masingini ili kurejesha uhalisia na haiba iliyokuwepo hapo awali katika eneo hilo.

11. Katika kuhakikisha Wizara inatekeleza agizo la Mheshimiwa Raisi wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, juu ya matumizi ya mfumo wa Kielektroniki katika kukusanya mapato, Kamati inaishauri Wizara kuharakisha matumizi ya mfumo huu katika misitu yote ya hifadhi wenye lengo la kuzuia upotevu wa mapato ya Serikali yatokanayo na msitu hiyo.

12. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji Maliasili na Mifugo kuujenga upya mnara uliopo katika msitu wa Masingini na kuhakikisha kuwa, unakua katika uhalisia wake. Mnara huu ni moja ya kivutio kikubwa kwa wageni kilichopo katika msitu huu.

**PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MIFUGO.**

Programu kuu hii inajumuisha programu ndogo moja ambayo ni ya Uzalishaji na Utibabu wa Mifugo pamoja na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (ZARILI).

**ZIARA ZA KAMATI KUANGALIA MAENDELEO YA PROGRAMU HII.**

Kamati katika kazi zake ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali kukagua Miradi ya maendeleo kwa lengo la kutathmini maendeleo yake pamoja na tija iliyopatikana. Kupitia programu hii Kamati ilifanya ziara katika maeneo yafuatayo: -

i) Chinjio la Wanyama – Mkoani na Wete;
ii) Mradi wa ujenzi wa Miundombinu ya Kituo cha Karantini ya Mifugo - Nziwenge- Gando Pemba;
iii) Taasisi ya Utafiti wa Mifugo;
iv) Kituo cha Utafiti wa Mifugo -Chamanangwe –Pemba;
v) Maabara ya Mifugo – Wete;
vi) Kituo cha Mifugo Magome Pemba na Kituo cha Utibabu wa Mifugo Meli Saba Unguja na
vii) Jumuiya ya Wafugaji wa Ng’ombe wa Maziwa (Uchozini Cooperative society).

**ZIARA KATIKA CHINJIO LA WANYAMA– MKOANI NA WETE (PEMBA)**

Kamati pia ilipata nafasi ya kufanya ziara yake katika machinjio ya wanyama yaliopo Mkoani na Wete kisiwani Pemba, kwa lengo la kuangalia hali halisi ya machinjio hayo.

Katika ziara yake hii, Kamati ilibaini uwepo wa changamoto zifuatazo ambazo kwa kiasi kikubwa zinakwamisha utekelezaji wa shughuli za kila siku katika machinjio hayo. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na;

1. Kamati ilijionea maeneo yanayotumika kama machinjio ya wanyama ambayo kiuhalisia ni maeneo madogo yaliyokosa vigezo na miundombinu mingi muhimu kwa utekelezaji wa shughuli ya uchinjaji wa wanyama hao. Kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa mbele ya Kamati ni kwamba, maeneo hayo yana uwezo wa kuchinja ng'ombe wawili hadi watatu (chinjio la Mkoani, ng'ombe wawili na chinjio la Wete, ng'ombe watatu) hali hii inapelekea serikali kukosa mapato ya uchinjaji hasa kwa siku za msimu wa sikukuu za kitaifa, ambapo wananchi wengi huhitaji huduma hii lakini hushindwa kuyatumia machinjio haya na badala yake huishia kuchinja wanyama hao katika sehemu zisizo rasmi.

2. Kamati pia ilibaini changamoto ya ukosefu wa ngoweko ***'hooks'*** za kuwekea nyama kwa lengo la kuiacha nyama ijichuje damu hali inayowalazimu wachinjaji kuiweka nyama hiyo juu ya baraza jambo ambalo ni hatari na si utaratibu unaofaa.

3. Changamoto nyengine ambayo Kamati imeibaini ni kukosekana kwa huduma ya umeme katika chinjio la Mkoani. Changamoto hii hukwamisha zoezi zima la kukagua na kuchinja ng'ombe wakati wa usiku pale inahitajika kufanya hivyo, hali inayopelekea usumbufu mkubwa kwa wafugaji wetu.

4. Pamoja na changamoto hizo, Kamati pia ilibaini ukosefu wa tenki la kuhifadhia maji katika chinjio la Mkoani. Kwa sasa maji yanayotumika kituoni hapo yanahifadhiwa katika hodhi moja ambalo halitoshelezi kwani endapo maji hayo yataisha usumbufu mkubwa huwapata wafanyakazi katika kituo hicho.

5. Kamati pia ilielezwa changamoto ya kukosekana kwa uzio katika machinjio hayo, ambapo kwa sasa uzio uliopo katika chinjio la Mkoani ni dhaifu hasa tukizingatia nguvu kubwa walizonazo wanyama wanaopelekwa chinjioni hapo, wengi wao huuharibu uzio huo.

6. Kuchimbuka kwa maji katika shimo linalotumika kuhifadhia mabaki na viungo visivyohitajika kwa wanyama wanaofika kuchinjwa katika chinjio Wete ni changamoto nyengine ambayo wafanyakazi katika chinjio hili hulazimika kufanya kazi ya ziada kwa kukusanya mabaki hayo katika sehemu isiyo rasmi jambo linahatarisha afya za wafanyakazi hao pamoja na wananchi wetu kwa ujumla.

7. Changamoto nyengine ambayo Kamati imebaini ni uchafu pamoja na harufu mbaya katika chinjio la Wete, hali inayoweza kuathiri afya za wananchi hasa tukizingatia kwamba, chinjio lipo karibu sana na eneo ambalo wavuvi hulitumia katika shughuli za kujitafutia riziki zao.

8. Katika chinjio la Wete, Kamati pia ilibaini changamoto ya kutofuatwa kwa utaratibu wa kawaida uliowekwa kwa wanyama kuwekwa kituoni hapo kwa muda wa masaa ishirini na nne kabla ya kuchinjwa.

9. Mafuniko ya mashimo yanayotumika katika kuhifadhia mabaki na viungo visivyohitajika kwa matumizi ya wanaadamu kwa wanyama wanaofika kuchinjwa katika chinjio la Wete, hayako rafiki kwa usalama wa wananchi wanaozunguka katika eneo hilo.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuanzisha mradi maalumu wa kuweka chinjio kubwa na la kisasa kisiwani Pemba kwa lengo la kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kutafuta vifaa vyote muhimu vinavyohitajika katika machinjio yaliyopo hivi sasa kisiwani Unguja na Pemba kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya kila siku

pamoja na kuiweka nyama inayochinjwa katika hali ya usafi na usalama.

3. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuharakisha uwekaji wa huduma ya umeme katika chinjio la Mkoani kutokana na umuhimu wake, lengo hasa ni kuwawezesha watendaji wetu kuweza kutekeleza majukumu yao muda wowote pale inapohitajika.

4. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagilaiji, Maliasili na Mifugo kuongeza idadi ya matenki yeye ujazo mkubwa wa kuhifadhia maji katika machinjio yaliyopo nchini kwa lengo la kumaliza kabisa changamoto ya maji iliyopo.

5. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuweka uzio madhubuti katika machinjio yaliyopo kwa lengo la kuwahifadhi wanyama wanaofika kuchinjwa katika vituo hivi.

6. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kutafuta sehemu maalumu ya kutupa mabaki yasiyohitajika yatokanayo na wanyama wanaochinjwa kwa lengo la kuziweka salama afya za wananchi waanaoishi katika maeneo ya jirani.

7. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kupitia Idara ya Mifugo kudumisha usafi katika machinjio yetu ili kuziweka salama afya za watumiaji na wanachi kwa ujumla.

8. Kutokana na umuhimu wa utaratibu wa kawaida uliowekwa kwa wanyama kuwekwa kituoni kwa muda wa masaa ishirini na nne kabla kuchinjwa, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuendelea na kuutekeleza utaratibu huo kwa lengo la kumlinda mtumiaji na kujiepusha na maradhi.

9. Kutokana na hali mbaya ya ufuniko wa shimo la kuhifadhia mabaki ya wanyama yasiyohitajika katika chinjio la Wete, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo

kuchukuwa hatua za haraka za kuirekebisha hali hii ili kuepusha athari mbaya zinazoweza kutokea.

10. Pamoja na hali hii, Kamati inaipongeza Wizara ya Kilimo kwa kutekeleza huduma zote za ukaguzi wa wanyama tangu wanapofika vituoni hadi kuchinjwa bila ya kuwasubiri Baraza la Mji ingawa wao wanaonekana kuwa ndio wasimamizi wakuu wa masuala haya.

## MRADI WA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA KITUO CHA KARANTINI YA MIFUGO (NZIWENGE- GANDO PEMBA)

Kamati ilipata nafasi ya kutembelea Mradi wa ujenzi wa Miundombinu ya Karantini ya Mifugo Gando na kujionea hali halisi ya utekelezaji wa mradi huu. Mradi ulianza rasm tokea mwaka 2018 kwa thamani ya shilingi za kitanzania Milioni Mia Tano, ukilenga kudhibiti uingiaji wa maradhi ya mifugo kutoka nje ya kisiwa cha Pemba. Eneo la Mradi linakadiriwa kuwa na ukubwa wa hekari 62.

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA UTEKELEZAJI WA MRADI HUU

Katika ziara yake hii Kamati ilibaini changamoto kadhaa ambazo kwa njia moja ama nyengine zilikwamisha utekelezaji wa mradi huu. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama hizi zifuatazo:

1. Hadi Kamati inafika katika eneo la Mradi, Kituo hiki bado hakijaanza kazi. Kamati imesikitishwa sana na hali hii hasa tukizingatia umuhimu wake na thamani ya fedha nyingi zilizotumika katika utekelezaji wa mradi huu na matokeo yake bado hayajaonekana. Kamati ilielezwa kwamba mradi ulilenga kutekeleza miundombinu ya kituo ikiwa ni pamoja na ujenzi wa ofisi, uchimbaji wa kisima, hodhi la kuhidhia maji na ujenzi wa uzio.
2. Kamati imebaini miundombinu isiyoridhisha katika kituo hiki. Kamati ilijionea kwa macho yake hali halisi ya mageti yaliyoanza kupoteza haiba yake kutokana na athari za hali ya hewa kisiwani hapa. Aidha Kamati ilielezwa changamoto ya ukosefu wa maji katika kisima kilichochimbwa katika kituo hiki, ubovu na ufinyu wa barabara ya kuingilia katika eneo la kituo, ukosefu wa huduma ya umeme pamoja na usalama mdogo katika hodhi la kuhifadhia maji liliopo katika kituo

hicho. Hodhi linaonekana kukosa hata mfiniko hali inayoweza kuhatarisha usalama wa wananchi waishio karibu na eneo hilo.

3. Kamati imebaini changamoto ya ushirikishwaji mdogo kwa maafisa toka kisiwani Pemba kwa ile miradi iliyowazunguka. Tunalithibitisha hili kutokana na ukweli kwamba, taarifa nyingi za mradi huu hazitambuliki kwa maafisa waliopo kisiwani Pemba. Hii inaonesha wazi kwamba shughuli zote za utekelezaji wa mradi huu ziliratibiwa makao makuu Unguja. Kamati inaliona suala hili kuwa si sahihi na ni kuwanyima fursa ya uwajibikaji maafisa hawa.

4. Kamati pia imebaini kukosekana kwa maandiko baina ya mmiliki wa eneo linalotarajiwa kujengwa banio la kuwadhiti wanyama kuelekea katika karantini. Changamoto hii inaweza kuibua mgogoro hapo baadae endapo Wizara haitachukuwa hatua za haraka.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati imeonesha masikitiko yake makubwa juu ya hali halisi ya Karantini hii kwamba, hadi Kamati inafika katika eneo hili ambapo ni takribani mwaka wa nee sasa, mradi huu bado haujaanza kazi. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kutilia maanani thamani kubwa ya fedha zinazotumika katika kutekeleza miradi kama hii na kuhakikisha kwamba, miradi hii inakuwa endelevu na kuleta tija kwa jamii iliyokusudiwa.
2. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kufanya tathmini na kuridhika na miradi yote inayotekelezwa chini ya Wizara hii, kabla ya kuipokea. Mradi huu wa ujenzi wa miundombinu ya kituo cha Karantini ya wanyama ulihusisha ujenzi wa ofisi, uchimbaji wa kisima, hodhi la kuhifadhia maji na ujenzi wa uzio, ambapo Kamati haikuridhika na utekelezaji wake kutokana na kutofikiwa kwa malengo yake.
3. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuhakikisha

kwamba watendaji kisiwani Pemba wanashirikishwa kikamilifu katika utekelezaji wa miradi inayowahusu. Utekelezaji wa suala hili utasaidia sana katika kuwajengea watendeji hawa morali pamoja na uzoefu katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

4. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kuharakisha uwekaji wa kumbukumbu za kimaandishi kati yake na mmiliki wa eneo linalotarajiwa kujengwa banio la kuwadhibiti wanyama kuelekea katika karantini hiyo, lengo ni kuepusha migogoro inayoweza kutokea hapo baadae.

5. Pamoja na yote hayo, Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wa mradi huu kutokana na ukweli kwamba, Wizara haikutoa kipaumbele cha kuuendeleza mradi huu. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati, fedha za mradi huu ziliingizwa katika bajeti ya mwaka 2018 na hadi Kamati inafika katika eneo la mradi, hakuna fedha yoyote iliyoingizwa kwa mradi huu muhimu unaogusa moja kwa moja maisha yetu.

## TAASISI YA UTAFITI WA MIFUGO (ZARILI)

Taasisi hii ilianzishwa kwa Hati ya Sheria (Legal Notice) nambari 45, chini ya kifungu 53 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na kifungu cha 55 cha Sheria ya Utumishi wa Umma Nambari 2 ya mwaka 2011. Lengo la kuanzishwa kwa taasisi hii ni kuendeleza tafiti za mifugo na kuimarisha sekta ya Mifugo nchini.

## CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI TAASISI YA UTAFITI WA MIFUGO (ZARILI)

Katika ziara yake hii, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo, ambazo kwa njia moja au nyengine zinakwamisha maendeleo ya taasisi hii.

1. Uhaba wa watafiti ni changamoto kubwa iliyoelezwa mbele ya Kamati ambayo taasisi hii inakabiliana nayo. Tukirejelea lengo la kuanzishwa kwa taasisi hii, Kamati inaliona jambo hili kuwa si rafiki kuwepo kituoni hapa.

2. Chamgamoto nyengine ambayo ilielezwa mbele ya Kamati ni ile ya kuchelewa kwa ujenzi wa miundombinu ya tafiti ambako kumechangia sana kuzorota kwa shughuli za kiutafiti katika taasisi hii.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Utafiti ndio nyenzo muhimu ya kufikia maendeleo katika sekta yoyote ile nchini, hivyo Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kulichukulia umuhimu mkubwa suala la kuipatia taasisi hii watafiti wa kutosha na wenye ujuzi kwa lengo la kuzisimamia shughuli za kiutendaji kwa manufaa makubwa.

2. Kamati inaipongeza taasisi hii kwa hatua kubwa ya maendeleo yaliyopatikana kutokana na tafiti mbalimbali zilizofanyika tangu kuanzishwa kwake na kuweza kuyafanikisha haya katika mazingira magumu ya uhaba wa watafiti na wataalamu. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kulifuatilia suala la ujenzi wa miundombinu ya tafiti ambayo utekelezaji wake umeanza kwa muda mrefu na hadi sasa utekelezaji wake si wa kuridhisha.

3. Kamati pia inaishauri Wizara kupitia taasisi hii kutoa elimu ya kutosha kwa wafugaji wetu ili waweze kufuga kitaalamu zaidi na waache kufuga kwa mazoea.

4. Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na taasisi hii kuhakikisha kuwa, matokeo ya tafiti zinazofanywa yasiishie vitabuni tu, bali yawafikie walengwa ambao ni wafugaji na waweze kuyatumia matokeo hayo katika kuzalisha zaidi.

## KITUO CHA UTAFITI WA MIFUGO (CHAMANANGWE -PEMBA)

Ni moja mwa vituo vya Utafiti wa mifugo viliopo chini ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo

Zanzibar katika Wizara ya Kilimo. Kituo hiki cha kisasa kina ukubwa wa eneo wa ekeri 63 ambazo zinatumika kwa shughuli mbalimbali za taasisi.

## CHANGANOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA KITUO HIKI

Katika ziara yake hii Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:

1. Upatikanaji mdogo wa fedha ni tatizo linalokwamisha utekelezaji wa kazi na malengo ya taasisi hii, ikiwa ni pamoja na kukwama kwa tafiti zilizopangwa kufanyika kwa wakati. Maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati yalithibitisha hali hii, ambapo jumla ya tafiti nne zilishindikana kufanyika kutokana na tatizo hili la ukosefu wa fedha.

2. Ukosefu wa mabanda kwa ajili ya kufanyia tafiti za ng'ombe na mbuzi kunakosababishwa na ukosefu wa fedha ni changamoto nyengine, ambayo inakwamisha juhudi za kufikia malengo ya kituo hiki.

3. Kamati imebaini changamoto ya ukosefu wa ofisi katika kituo hiki, hali inayorudisha nyuma morali ya kiutendaji kwa wafanyakazi waliopo. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati, taratibu za kumpata mkandarasi na michoro ya ujenzi wa ofisi hii tayari zimeshafanyika na mkandaraasi tayari ameshapatikana lakini hadi Kamati inafika katika kituo hiki, ujenzi huo bado haujaanza.

4. Upungufu mkubwa wa watafiti kituoni hapo ni changamoto inayorudisha nyuma malengo ya kuanzishwa kituo hiki. Kituo kina jumla ya watafiti 6 tu ambao ni wenye kiwango cha Cheti na Diploma.

5. Hati miliki ya eneo hili bado haijapatikana kutokana na tatizo la ukosefu wa fedha.

6. Kiangazi cha muda mrefu ni changamoto nyengine iliyoelezwa mbele ya Kamati kinachosababisha uzalishaji mdogo wa malisho na kuathiri afya na uzalishaji wa mifugo.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kutokana na umuhimu wa tafiti katika kukiendeleza kituo cha Utafiti wa Mifugo kisiwani Pemba, Kamati inaishauri Wizara kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha kituo kinaingiziwa fedha za bajeti kwa wakati kwa lengo la kukiwezesha kituo hiki kufikia malengo ya kuanzishwa kwake.

2. Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Kilimo kushirikiana na Wizara ya Fedha, kuwapatia kituo hiki fedha za kutosha na kwa wakati ili waweze kufanikisha utekekelezaji wa shughuli za kituo kwa ufanisi.

3. Kutokana na umuhimu wa kuwepo kwa mabanda kwa ajili ya kufanyia tafiti za ng'ombe na mbuzi kituoni hapo, Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Kilimo kushirikiana kikamilifu na Wizara ya Fedha na Mipango, kuhakikisha wanawaingizia fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabanda hayo, ili ujenzi huo uweze kufanikiwa na tafiti kwa ajili ya wanyama hao ziweze kuendelea kama ilivyopangwa.
4. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kujenga jengo kwa ajili ya ofisi, ambalo litarejesha morali ya kiutendaji kituoni hapo.
5. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Utumishi wa Umma kuongeza idadi ya wataalamu kituoni hapo, kwa kuwaajiri wataalamu wenye viwango vya juu vya elimu ili, tafiti zinazopangwa ziweze kutekelezeka kwa ufanisi mkubwa. Likifanikiwa hili, Kituo kitaweza kuwa mfano kwa kutoa mifugo iliyobora na wafugaji wanaofika kituoni hapo wataweza kujifunza kivitendo.

6. Wizara ya Kilimo ijitahidi kukipatia fedha kituo hiki, ili suala la upatikanaji wa hati miliki liweze kukamilika.
7. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kupita Kituo cha Utafiti wa Mifugo, kuongeza uzalishaji wa malisho ya wanyama katika miongo mengine isiyo ya kiangazi ili kuweza kujiwekea hakiba ya kutosha itakayoweza kutumika katika msimu wa kiangazi, ambapo hali ya uzalishaji wa malisho unaonekana kupungua kwa sababu ya jua kali.

## MAABARA YA MIFUGO – WETE

Maabara hii imeanzishwa mwaka 2013 kwa lengo la kuongeza ufanisi kwa madaktari na

wataalamu wa mifugo katika kuyatambua magonjwa yanayosababishwa na vimelea vya aina mbalimbali kwa kufanya uchunguzi wa sampuli na majaribio ya matumizi ya madawa, kuweza kutambua aina bora ya dawa miongoni mwa madawa ya jamii inayoweza kutibu kwa uhakika zaidi kabla ya kuendelea na kutoa huduma za matibabu na kuepuka kufanya matumizi ya madawa kwa kubahatisha.

## MAFANIKIO YA MAABARA YA MIFUGO

1. Maabara imefanikiwa kuchunguza na kutambua magonjwa ya Parasitology (Protozoa, Minyoo na Mange) kufanya uchunguzi kwa kuangalia ubora wa mbegu kwa kupandishia Ngombe kwa sindano.

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

1. Kamati imebaini changamoto ya udogo (ufinyu) wa jengo ambalo linashindwa kukidhi shughuli za kiutendaji kama Maabara, jambo linalorudisha nyuma kasi ya maendeleo kituoni hapo.

2. Kuharibika kwa kifaa muhimu (incubator) cha kufanyia uchunguzi wa maradhi kituoni hapo ni changamoto nyengine ambayo Kamati imeibaini. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati, kifaa hii kimeharibika tokea mwaka 2020 na hadi sasa bado matengenezo yake hayajafanikiwa, hali inayokwamisha utekelezaji mzuri wa shughuli katika maabara hii.

3. Lengo kuu la kuanzishwa kwa maabara hii ni kufanya uchunguzi wa magonjwa mbalimbali yanayowashambulia mifugo. Kamati imebaini kuwa lengo hili linashindwa kutekelezeka kutokana na upungufu mkubwa wa wataalamu uliopo katika maabara hii. Kamati ilielezwa kuwa ni wafanyakazi watatu tu ndio waliopo kwa sasa katika maabara hii, hali inayorudisha nyuma kasi ya maendeleo katika kuipeleka mbele sekta hii ya mifugo nchini.

4. Changamoto nyengine iliyoelezwa mbele ya Kamati ni ile ya uhaba wa fedha katika ufuatiliaji wa mwenendo wa magonjwa kwa wafugaji.

5. Elimu ndogo waliyonayo wafugaji ni changamoto nyengine iliyobainika. Kwa

mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati ni kwamba, wafugaji walio wengi ni wenye kubadilika badilika na hawana elimu ya kutosha katika tasnia hii, hali inayopelekea mifugo mingi kuathirika na magonjwa na kupelekea uzalishaji mdogo.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kutokana na hali ya jengo lilivyo hivi sasa, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kutafuta uwezekano wa kujenga jengo jengine la kisasa litakaloweza kutoa huduma kwa ufanisi mkubwa zaidi.
2. Kamati ilielezwa kwamba, bajeti ya manunuzi ya kifaa cha kufanyia uchunguzi ***(incubator)*** katika maabara hii tayari ipo hivyo, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuharakisha mchakato wa manunuzi ya kifaa hiki muhimu kwa lengo la kupeleka mbele maendeleo ya maabara hii muhimu sana kwa wafugaji wetu.
3. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kushirikiana na Wizara ya Utumishi wa Umma kuhakikisha kwamba inaongeza idadi ya wafanyakazi wenye sifa zinazofaa na kuhitajika katika kuipeleka mbele maabara hii katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku.
4. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuwaingizia Maabara hii fedha za OC kwa wakati ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.
5. Katika kuhakikisha kwamba wafugaji wanajikinga na magonjwa yanayoshambulia mifugo, ikiwa ni pamoja na magonjwa ya kiwele ambayo hupelekea uzalishaji mdogo wa maziwa, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, kuendelea kutoa elimu zadi kwa wafugaji wetu juu ya matumizi ya malisho yaliyo bora kwa mifugo yao ambayo yatachochea uzalishaji ulio bora zaidi.

## KITUO CHA UTIBABU WA MIFUGO MAGOME - PEMBA

Kituo cha Utabibu wa Mifugo Magome, kilianzishwa mnamo mwaka 1975 kwa ajili ya

shughuli za upandishaji ng'ombe kwa sindano, ukusanyaji wa mbegu pamoja na uhifadhi wake kwa kisiwa chote cha Pemba.

## MAFANIKIO YA KITUO CHA UTIBABU WA MIFUGO MAGOME – PEMBA

1. Jumla ya wafugaji 250 wamepatiwa taalum za aina mbali mbali juu ya ufugaji bora kuanzia mwezi January 2022 kituo kilipoanza kufanya kazi.
2. Jumla ya mifugo ipatao 385 imepatiwa huduma za matibabu zidi ya magonjwa mbali mbali.

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

Kamati katika ziara yake hii ilibaini changamoto zifuatazo:

1. Kamati imeelezwa changamoto ya uhaba wa wafanyakazi katika kituo hiki. Kwa sasa kituo kina wafanyakazi watatu tu jambo linalozorotesha utekelezaji wa majukumu katika kituo hiki.

2. Kamati pia imeelezwa changamoto ya usafiri inayowakabili wafanyakazi katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku.

3. Kukosekana kwa miundombinu ya maji na umeme katika kituo hiki ni changamoto nyengine iliyoelezwa mbele ya Kamati. Ni muda mrefu sasa kituo hiki kinatoa huduma bila ya kuwepo huduma hizi muhimu za kibinaadamu.

4. Kukosekana kwa uzio katika eneo la kituo hiki imeelezwa kuwa ni changamoto ya muda mrefu, ambapo kituo kipo tokea mwaka 1975 lakini hadi sasa eneo lipo wazi, hali inayoweza kutoa fursa kwa jamii iliyozunguka kituo hiki, kulitumia eneo kwa shughuli za kijamii.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuongeza idadi ya wafanyakazi katika kituo hiki hasa tukizingatia kwamba, kazi zinazofanywa na kituo hiki ni za ufuatiliaji, wafanyakazi hulazimika kuwafuata wafugaji nje ya kituo kwenda kuwapatia huduma.

2. Kutokana na mazingira halisi ya wafanyakazi katika kuteleleza majukumu yao, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuwapatia usafiri wa uhakika wafanyakazi wa ktuo hiki, ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa wepesi zaidi.

3. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuharakisha mchakato wa uingizaji wa huduma za maji na umeme, hasa tukizingatia umuhimu wake kwa jamii.

4. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuliwekea uzio eneo lote lililozunguka kituo ili kuepusha uvamizi utakaoweza kufanywa na wananchi.

## KITUO CHA UTIBABU WA MIFUGO MELI SABA (DARAJA LA SHENI) UNGUJA.

Kituo hiki kilianzishwa mwaka 1978 kikiwa na lengo la kutoa huduma za tiba na kinga kwa Wanyama, kutoa huduma za upandishaji wa ng'ombe kwa sindano pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji.

## MAFANIKIO YA KITUO CHA UTIBABU WA MIFUGO MELI SABA (DARAJA LA SHENI) - UNGUJA.

1. Kitio kimefanikiwa kutoa huduma za kinga na tiba.
2. Kituo kimefanikiwa kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji
3. Kituo kimefanikiwa kutoa huduma ya upandishaji Ng'ombe kwa sindano kupitia

maafisa mifugo wastaafu na vijana maalumu waliopatiwa mafunzo hayo.

4. Kituo kimefanikiwa kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji Katika kuchanja mifugo yao kwa wakati muafaka.
5. Kituo kimefanikiwa kutoa huduma za kinga dhidi ya maradhi ya mlipuko kwa kutoa chanjo cha kichaa cha mbwa (RABIES VACCINE)

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

1. Kamati imebaini changamoto kubwa ya ukosefu wa vitendea kazi katika kituo hiki. Karani wa kituo hiki anafanya kazi zake kwa kutumia njia zilizopitwa na wakati.
2. Changamoto ya ukosefu wa hati miliki ya kituo hiki pia ilielezwa mbele ya kamati, hali inayoweza kutoa fursa kwa wananchi kulivamia eneo kwa shughuli za kijamii.

3. Changmoto nyengine ambayo ilielezwa mbele ya Kamati ni ile ya ukosefu wa huduma muhimu ya maji katika kituo hiki.

4. Aidha, usafiri ni changamoto nyengine iliyobainika ambapo ilielezwa kuwa, hakuna usafiri rasm kituoni hapo na wafanyakazi hutumia usafiri usiorasmi katika kuwafuata wafugaji kuwapatia huduma na wafugaji hulazimika kugharamia usafiri kwa wafanyakazi hao.

5. Changamoto ya uhaba wa walinzi katika kituo hiki ni changamoto nyengine iliyoelezwa mbele ya Kamati. Ni walinzi wawili tu waliopo ambao kwa sasa hawakidhi mahitaji.

6. Changamoto nyengine iliyoelezwa mbele ya Kamati ni ile ya uchache wa wataalamu wanaotumika katika kutoa huduma katika kituo hiki. Kamati ilielezwa kuwa, Kituo kimezungukwa na Shehia 32, ambapo Kituo kimefikia maamuzi ya kuwatumia wastaafu katika kutoa huduma ya upandishaji wa ng’ombe kwa sindano.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Katika kuhakikisha kwamba kituo hiki kinaimarika na kinakwenda sambamba na maendeleo ya sayansi na teknoljia yaliyopo duniani hivi sasa, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuwapatia wafanyakazi wa kituo hiki, mashine za kisasa ikiwa ni pamoja na komputa, katika kuteleleza majukumu yao ya kila siku.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuharakisha upatikanaji wa hati miliki ya kituo hiki hasa tukizingatia kituo ni cha muda mrefu sasa, hii itaweza kusaidia katika kuepusha uvamizi na migogoro kati ya wananchi na Serikali hapo baadae.

3. Sote ni mashahidi kuwa maji ni uhai, basi ni vyema kwa Wizara ya Kilimo kupitia Idara yake ya Mifugo, kuwapatia Kituo hiki huduma hii muhimu kwa matumizi yao ya kila siku. Aidha, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kukibadilisha Kituo hiki na kuwa Kituo cha kisasa kabisa kwa kukiwekea miundombinu sahihi itakayowawezesha wafanyakazi kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

4. Kupitia hali hii, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuwapatia usafiri wa uhakika wafanyakazi wa kituo hiki ili waweze kuondokana na usumbufu wanaoupata hivi sasa.

5. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kushirikiana na Wizara ya Utumishi wa Umma kuongeza idadi ya wafanyakazi wakiwemo walinzi na wataalamu wa kutoa huduma katika kituo hiki, kwa kupeleka maombi ya ajira katika Wizara ya Utumishi wa Umma. Aidha, Kamati inawapongeza wastaafu kwa moyo wao wa kizalendo walioonesha katika kushirikiana na wafanyakazi waliopo katika kuhakikisha kwamba, huduma za upandishaji wa ng'ombe kwa sindano katika Kituo hiki zinatolewa kama kawaida.

6. Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuwasomesha vijana katika tasnia hii ya Mifugo ili kuweza kuziba pengo la upungufu mkubwa wa wafanyakazi uliopo hivi sasa katika vituo vyote nchini.

7. Vilevile, Kamati inaipongeza Wizara ya Kilimo kwa kuwashirikisha Wadau wote

wa mifugo katika mabadiliko ya tozo kwa huduma zinazotolewa kituoni hapo. Kamati inaamini kuwa, hatua hii itaweza kuendeleza umoja na mshikamano kati ya Wizara na Wadau hao katika kutekeleza majukumu ya kila siku.

8. Kamati inawapongeza wafanyakazi wote wa Kituo hiki kwa jinsi wanavyojitoa katika kuwasaidia wafugaji wetu katika kuwapatia huduma za ushauri, elimu na kuwawezesha kufuga kitaalamu zaidi.

9. Kamati inaupongeza uongozi wa Kituo hiki kwa kuanza kuutumia mfumo wa kielekroniki katika ukusanyaji wa mapato kama agizo la Serikali linavyoelekeza, hii itasaidia sana katika upotevu wa mapato ya Serikali.

## JUMUIYA YA WAFUGAJI WA NG'OMBE WA MAZIWA (UCHOZINI COOPERATIVE SOCIETY)

Kamati ilipata nafasi ya kuonana na Jumuiya ya Wafugaji wa Ng'ombe wa Maziwa (*Uchozini Cooperative Society)* na kujionea hali halisi ya maendeleo katika harakati za ufugaji wao.

Jumuiya hii imesajiliwa rasmi kwa hati ya ushirika No. P 997/99 ya tarehe 9/6/1999 ikiwa na lengo la kujiajiri wenyewe kupitia shughuli hii ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa kwa madhumuni ya kuzalisha na kuuza, ng'ombe, maziwa pamoja na mazao mengine yatokanayo na mifugo. Shughuli hizi za ufugaji zinafanyika katika shamba la Fueni linalomilikiwa na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo.

## MAFANIKIO YA JUMUIYA YA WAFUGAJI WA NG'OMBE WA MAZIWA (UCHOZINI COOPERATIVE SOCIETY)

1. Jumuiya imefanikiwa kuboresha hali zao kimaisha.

2. Shughuli zao za ufugaji zimewasaidia sana katika upatikanaji wa ajira, jumla ya

watu 26 wanafanyakazi za kutoa huduma katika shamba hilo.

3. Ufugaji wa ngombe katika shamba hilo umesaidia sana katika utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti ya kudumu kwenye mipaka na maeneo ya maporomoko ya udongo.

## CHANGAMOITO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

Katika ziara yake hii Kamati ilibaini changamoto zifuatazo ambazo kwa njia moja au nyengine zinachangia kurudisha nyuma kasi ya maendeleo katika Jumuiya hii. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:

1. Kamati ilielezwa changamoto ya baadhi ya watu binafsi na taasisi nyengine zenye uwezo, kutaka kulitumia eneo hili katika kuwekeza miradi ya kijamii kama vile viwanja vya kufurahishia Watoto na kuitishia Jumuiya hii juu ya kutoendelea kulitumia eneo la shamba hili katika harakati zao za ufugaji. Hii ni changamoto iliyoelezwa mbele ya Kamati ambayo kwa kiasi kikubwa inarudisha nyuma kasi waliyonayo wafugaji hawa hasa tukizingatia mtaji mkubwa wa fedha waliokwishauwekeza katika harakati zao hizi.

2. Kamati imebaini changamoto ya upungufu mkubwa wa ***liquid Nitrogen gas*** uliopo hivi sasa, inayotumika katika upandishaji wa ng'ombe kwa sindano. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati ni kwamba, hapo nyuma zoezi la upandishaji wa ng'ombe kwa sindano lilikuwa likifanywa na Serikali lakini kwa hivi sasa wafugaji wanalazimika kugharamia wenyewe, jambo linalorudisha nyuma kasi ya uzalishaji wa mbegu bora za mifugo kutokana na uwezo mdogo walionao wafugaji hao.

3. Kamati imebaini changamoto kubwa ya ukosekanaji wa mikopo kwa wanajumuiya kutoka katika taasisi za kifedha zilizoidhinishwa na Serikali kuwapatia mikopo wajasiriamali, hali inayorudisha nyuma kasi ya maendeleo yao. Wanajumuiya hawa walishusha tuhuma zao kwa CRDB benki, kuwa ndio kikwazo cha upatikanaji wa mikopo kwa wanajumuiya hawa.

4. Uchache wa maeneo ya malisho katika shamba kwa sasa ni changamoto

nyengine iliyoelezwa mbele ya Kamati, ambayo hayatoshelezi mahitaji ya malisho kwa ng'ombe waliopo jambo linalowalazimisha wafugaji kwenda kutafuta malisho katika sehemu nyengine.

5. Kamati pia ilielezwa changamoto ya soko la maziwa hasa kwa kipindi cha Kipupwe, ambapo maziwa huzalishwa kwa wingi.

6. Kamati imebaini kuwa wafugaji walio wengi hawana elimu ya kutosha juu ya kuendeleza shughuli zao na matokeo yake ni ufugaji usio na tija.

7. Bei kubwa ya pembejeo za mifugo ikiwa ni pamoja na madawa na chakula ni changamoto nyengine iliyoelezwa mbele ya Kamati ambayo kwa mujibu wa soko, zinamuweka mfugaji katika mazingira magumu kimaslahi.

8. Maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati yanathibitisha kwamba Idara ya Mifugo inakabiliwa na changamoto kubwa ya upungufu wa wafanyakazi. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati, kwa sasa Idara ya Mifugo ina mtaalamu mmoja tu, ambaye kitaalamu hawezi kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Wataalamu wake wote tayari wamestaafu.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaipongeza sana Wizara ya Kilimo chini ya uongozi wake Mheshimiwa Shamata Shaame Khamis, kwa maamuzi aliyoyatoa mbele ya Kamati kwa kuwatoa wasiwasi wafugaji hao na kuwaruhusu kuendelea kulitumia eneo la shamba hilo katika shughuli zao hizi muhimu kwa maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

2. Katika kuhakikisha kwamba tunawasaidia wafugaji wetu waweze kufuga kitaalamu na kuzalisha mifugo iliyo bora, Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Kilimo kuharakisha mchakato wa manunuzi wa Mtambo Mpya wa kuzalishia gesi ya kupandishia ng'ombe kwa sindano, kwa lengo la kuwaondolea usumbufu

uliopo hivi sasa wafugaji wetu na hasa tukizingatia Mtambo huu bajeti tayari imeshatengwa.

3. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kushirikiana na Wizara ya Uwezeshaji Kiuchumu, kuhakikisha wanajumuiya hawa wanapatiwa Mikopo kutoka katika Benki zilizopo nchini, ili waweze kujiendeleza katika ufugaji wao.

4. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na SMIDA kuwapatia wana jumuiya mashine ya kusindika maziwa na kuweza kuzalisha bidhaa zitokanazo na maziwa ili tija ya moja kwa moja iweze kupatikana.

5. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kuwapatia wafugaji fursa za mafunzo ya ndani na nje ya nchi, ili kuwawezesha kufuga kitaalamu zaidi.

6. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, kuwasaidia wafugaji hawa katika upatikanaji wa pembejeo za mifugo kwa lengo la kuwakwamua katika harakati zao za ufugaji.

7. Kutokana na upungufu mkubwa wa wataalamu katika Idara ya Mifugo, Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo kushirikiana na Wizara ya Utumishi wa Umma kuhakikisha inawaajiri vijana wenye sifa watakaoweza kujaza nafasi zilizo wazi.

8. Pamoja na yote hayo, Kamati inatoa pongezi zake za dhati kwa Jumuiya ya Wafugaji Ng'ombe wa Maziwa ***(Uchozini Cooperative Society)*** kwa hatua nzuri waliyoifikia ya kuongeza idadi ya wafugaji wa ng'ombe wa maziwa kutoka wafugaji 4 mwaka 1991 hadi kufikia wafugaji 13 mwaka huu 2023 kwa kumiliki ng'ombe 63.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA KILIMO.

Programu kuu hii ina jumuisha programu ndogo tatu

i) Programu ndogo ya Uendeshaji;

ii) Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti na

iii) Programu ndogo ya Uratibu wa kazi za Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo - Pemba.

## ZIARA ZA KAMATI KUANGALIA MAENDELEO YA PROGRAMU HII.

Kamati katika kazi zake ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali kukagua Miradi ya maendeleo kwa lengo la kutathmini maendeleo yake pamoja na tija iliyopatikana. Kupitia program hizi Kamati ilifanya ziara katika maeneo yafuatayo:

i) Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba.

## ZIARA KATIKA OFISI YA AFISA MDHAMINI- PEMBA

Ofisi ya Afisa Mdhamini ni ofisi yenye jukumu la kusimamia Idara zifuatazo;

i) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;

ii) Idara ya Uendeshaji na Utumishi;

iii) Idara ya Kilimo na Uhakika wa chakula;

iv) Idara ya Misitu,

v) Idara ya Umwagiliaji Maji; na

vi) Idara ya Maendeleo ya Mifugo.

Afisi hii pia inasimamia utekelezaji wa majukumu katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo pamoja na Wakala wa Matrekta na Zana za Kilimo.

Katika ziara yake hii, Kamati ilelezwa mambo mengi yakiwemo mafanikio na changamoto zinazoikabili Wizara katika kuzisimamia idara na taasisi hizi.

## MAFANIKIO KATIKA OFISI YA AFISA MDHAMINI- PEMBA

1. Wizara imefanikiwa kupata mashirikiano makubwa kutoka katika taasisi za watoa huduma binafsi pamoja na Mabwana na mabibi shamba kwa kuweza kuwatembelea wakulima wengi zaidi.

2. Wakulima wengi nchini wamefanikiwa kuzalisha mazao mbadala kama vile vitunguu maji pamoja na kuvuna mazao ya mbogamboga ambayo ni matokeo ya mafunzo ya nadharia waliyopatiwa kupitia jumuiya ya Hifadhi ya misitu ya jamii.

## CHANGAMOTO KATIKA OFISI YA AFISA MDHAMINI- PEMBA

Kamati katika ziara yake ilibaini changamoto zifuatazo: -

1. Kamati ilielezwa changamoto kubwa ya uhaba wa watumishi katika Taasisi zilizomo ndani ya Wizara hii hususani mabibi na mabwana shamba, hali inayopelekea ucheleweshaji katika kukamilisha majukumu ya taasisi hizo katika suala zima la usimamizi na kuwafikia wakulima kwa wakati kwa lengo la kuwapatia ushauri wa kitaalamu katika shughuli zao za uzalishaji.

2. Kamati pia ilielezwa changamoto kubwa ya maradhi na wadudu waharibifu wa mimea na matunda. Kamati ilielezwa kuwa kwa kiasi kikubwa maradhi na wadudu yamekuwa ni kikwazo kwa wakulima wetu kwa mazao yao huko mashambani jambo linalorudisha nyuma kasi ya uzalishaji.

3. Pia Kamati ilielezwa upungufu wa vifaa vya kutendea kazi katika Idara na Tasasisi zilizo chini ya Wizara hii jambo linalozorotesha utekelezaji wa majukumu ya kila siku na hatimae kutofikiwa kwa malengo yaliyopangwa na Wizara.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Serikali kuipatia Wizara hii wafanyakazi wa kutoka hasa mabibi na mabwana shamba kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya taasisi ziliopo chini ya Ofisi hii muhimu kisiwani Pemba. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuwapatia motisha wafanyakazi wake kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yao.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kutafuta mbinu mbadala za kuzuia maradhi ya wadudu waharibifu wa matunda na mazao mbali mbali ya wakulima ili kuepusha hasara kubwa wanayoipata wakulima wetu. Aidha Wizara ya Kilimo ijikite katika kufanya tafiti zinazohusiana na wadudu waharibifu wa matunda ambao wanaendelea kuyaharibu mazao siku hadi siku. Vilevile Wizara ifanye tafiti juu ya uzalishaji mdogo kwa wakulima wetu na matokeo ya tafiti hizi yawafikie wakulima wetu ili waweze kubadilika na kuzalisha kilimo chenye tija chini ya uangalizi na ufuatiliaji wa Wizara.

3. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuzipatia idara na taasisi zetu vitendea kazi vya kutosha ili wafanya kazi hawa waweze kwenda sambamba na kasi ya mabadiliko katika kuzalisha kilimo cha kisasa na chenye tija kwa manufaa yao binafsi na taifa kwa ujumla.

## WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda inaundwa na Idara na taasisi mbali mbali ambazo kwa pamoja zina lenga kutoa huduma kwa wananchi wote bila ubaguzi wowote.

## IDARA ZA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

1. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
2. Idara ya Sera na Utafiti
3. Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko
4. Idara ya Maendeleo ya Viwanda
5. Afisi ya Afsa Mdhamini Pemba.

## TAASISI NA MASHIRIKA YA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA

1. Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC)
2. Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali
3. Baraza la Taifa la Biashara (ZNBC)
4. Taasisi ya Viwango zanzibar (ZBS)
5. Mamlaka ya Usimamizi wa leseni
6. Wakala wa Maendeleo ya Viwanda Vidogo vidogo, vidogo na vya Kati (SMIDA)
7. Tume ya Ushindani Halali wa Biashara
8. Baraza la Ushindani wa Biashara
9. Wakala wa Vipimo.

**PROGRAMU KUU ZA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIAWANDA**

Wizara hii katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku inajiendesha kupitia Programu kuu zifuatazo:

i) Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda;
ii) Programu Kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali;
iii) Programu Kuu Ukuzaji na Uendelezaji wa Biashara;
iv) Programu Kuu ya Viwango na Tathmini ya Ubora

**PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA;**

Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda inasimamiwa na programu ndogo tatu kwa mujibu wa huduma zinazotolewa. Programu hizo ni:

i) Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji wa shughuli za Wizara,

ii) Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti za Wizara na

iii) Programu ndogo ya Uratibu na Utekelezaji wa Shughuli za Wizara Pemba.

## ZIARA ZA KAMATI KUANGALIA MAENDELEO YA PROGRAMU HII

Kamati katika kazi zake, ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali pamoja na kukagua Miradi ya maendeleo kwa lengo la kutathmini maendeleo yake pamoja na tija iliyopatikana. Kupitia programu ndogo hizi, Kamati ilifanya ziara katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:

i. Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba.

## OFISI YA AFISA MDHAMINI PEMBA

Kamati ilifanya ziara katika ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba na kupatiwa taarifa juu ya uendeshaji wa taasisi na Idara zilizo chini ya Ofisi hii. Miongoni mwa taasisi na idara hizo ni kama hizi zifuatazo:

a) Idara ya Utumishi na Uendeshaji;

b) Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;

c) Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko;

d) Idara ya Maendeleo ya Viwanda;

e) Idara ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali;

f) Wakala wa Mizani na Vipimo;

g) Wakala wa Viwanda Vidogovidogo, vidogo na vya Kati;

h) Tume ya Ushindanbi Halali wa Biashara (ZFCC);

i) Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) na

j) Taasisi ya Viwango (ZBS)

## MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KWA TAASISI NA IDARA ZILIZO CHINI YA OFISI YA AFISA MDHAMINI -PEMBA

Katika utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku, taasisi na idara hizi ziimefanikiwa kutekeleza majukumu yake kama ifuatavyo:

1. Kukagua maduka kwa Wilaya zote za Pemba ili kuhakikisha bei elekezi zilizotolewa na Serikali kupitia Wizara hii zinafuatwa na wafanya biashara.

2. Kutembelea wajasiriamali ili kujua changamoto zao zinazowakabili na kuwapatia ushauri elekezi.

3. Kuwatembelea wakulima wa mwani waliopatiwa mafunzo ya ukulima bora wa mwani aina ya Kotonii na Ulva ili kuona muendelezo wa ukulima huo katika maeneo ya Wingwi, Tumbe na Makangale.

4. Kusimamia mafunzo ya wajasiriamali ya umuhimu wa kujisajili na upatikanaji wa leseni kwa njia ya Mtandao.

5. Kutoa mafunzo juu ya uelewa wa ukulima bora na upatikanaji wa masoko kwa wakulima 300. Makangale 150, Tumbe 75 na Chokocho 75.

## CHANGAMOTO ZINAZOZIKABILI TAASISI NA IDARA ZILIZO CHINI YA OFISI YA AFISA MDHAMINI - PEMBA

Katika ziara yake hii Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:

1. Kamati ilielezwa changamoto ya uhaba wa wafanyakazi unaozikabili taasisi na Idara zilizomo katika Wizara hii ambapo Kamati ilielezwa kuwa, uhaba huo wa wafanyakazi unarudisha nyuma kasi ya utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

2. Changamoto nyengine iliyoelezwa mbele ya Kamati ni ufinyu wa bajeti inayopangwa na uingizwaji mdogo wa OC kwa idara na taasisi zilizopo kiswani Pemba, hali inayopelekea baadhi ya majukumu kushindwa kutekelezwa kama yalivyopangwa.

3. Aidha, Kamati ilibaini changamoto nyengine ya malimbikizo ya madeni kutoka kwa watoa huduma wa Wizara ambapo ilielezwa kuwa Wizara ina mrundikano wa madeni ya muda mrefu hadi sasa na bado hayajalipwa kwa wahusika.

4. Uhaba wa vyombo vya usafiri imeelezwa kuwa ni miongoni mwa changamoto inayozikabili Taasisi na Idara ziliomo katika Wizara hii kisiwani Pemba. Kamati ilifahamishwa kuwa vyombo vya usafiri vilivyopo ni vichache havikidhi mahitaji. Aidha, kwa upande wa magari mengi yao yamechakaa hali inayokwamisha utekelezaji wa kazi za taasisi hizo.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Serikali kuajiri nguvu kazi ya kutosha kwa idara na taasisi zilizo chini ya Ofisi hii kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya kila siku kwa taasisi hizi ili malengo ya serikali yaweze kutekelezwa kama yalivyopangwa.

2. Kamati inaishauri Serikali kuipangia bajeti ya kutosha Wizara hii muhimu na kuiingiza OC kwa Idara na Taasisi hizi kwa wakati ili majukumu yaweze kutekelezwa kama yalivyopangwa.

3. Pamoja na maelezo ya Wizara kuwa, kwa sasa madeni ya nyuma yanalipwa na Serikali Kuu kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina bado Kamati inasisitiza Wizara kuweka utaratibu mzuri wa kuyalipa madeni haya kwa awamu kulingana na

upatikanaji wa fedha.

4. Kamati inaishauri Serikali kuzipatia Taasisi na Idara hizi vyombo vya usafiri kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa majukumu kwa ufanisi.

5. Hata hivyo Kamati inachukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa upande wa Pemba kutokana na utekelezaji wake mzuri wa majukumu pamoja na kwamba kuna mgao mdogo wa fedha.

**PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA VIWANDA NA UJASIRIAMALI**

Programu kuu hii utekelezaji wake unasimamiwa na Idara ya Maendeleo ya Viwanda na Wakala wa Maendeleo ya Viwanda vidogovidogo, vidogo na vya Kati (SMIDA) ikijumuisha Programu ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya Ukuzaji Viwanda na Programu ndogo ya Maendeleo ya Ujasiriamali.

**ZIARA ZA KAMATI KUANGALIA MAENDELEO YA PROGRAMU HII.**

Kamati katika kazi zake, ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali pamoja na kukagua Miradi ya maendeleo kwa lengo la kutathmini maendeleo yake pamoja na tija iliyopatikana. Kupitia programu ndogo hizi Kamati ilifanya ziara katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:

i) Maeneo ya Uwekezaji - Dunga, Pangatupu, Chamanangwe;
ii) Maeneo yanayotarajiwa kujengwa viwanja vya maonesho –Nyamanzi;
iii) Kiwanda cha Maji - Kinyikani - Pemba;
iv) Kiwanda cha Mwani Chamanangwe – Pemba
v) Umoja wa Wazalishaji wa Asali - Machomane Chakechake Pemba;
vi) Kituo cha kuchakata Mazao ya Kilimo - Kizimbani Unguja;

**ZIARA KATIKA MAENEO YA UWEKEZAJI DUNGA, NYAMANZI, PANGATUPU NA**

CHAMANANGWE.

Kamati ilipata nafasi ya kufanya ziara katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda Dunga na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kufanyia maonyesho ya kibiashara Nyamanzi. Eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda Dunga lina ukubwa wa hekeri 61. 8 ambalo litahusisha ujenzi wa viwanda vidodgovidogo na vikubwa, kukamilika kwa mradi huu kutasaidia sana kupeleka mbele gurudumu la maendeleo ya nchi yetu.

Eneo la Nyamanzi linalotarajiwa kuwekwa maonyesho ya kibiashara nalo kwa upande wake lina ukubwa wa hekari 60, ambapo kukamilika kwa ujenzi wa mabanda ya kudumu ya maonyesho kutaipunguzia gharama kubwa Serikali pamoja na Wizara katika kuratibu shughuli za maenyesho pale wakati utakapowadia.

Eneo linalotarajiwa kujengwa viwanda Pangatupu ni eneo linalokadiriwa kuwa na ukubwa wa hekta 163 sawa na ekeri 407.

CHANGAMOTO KATIKA MAENEO YA UWEKEZAJI DUNGA, NYAMANZI, PANGATUPU, CHAMANANGWE

Katika ziara zake hizi, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:

1. Kamati imebaini changamoto ya miundombinu ya barabara isiyoridhisha kutoka barabara kuu hadi katika maeneo ya miradi hii, changamoto hizi zisipochuliwa hatua mapema basi zinaweza kukwamisha utekelezaji wa malengo ya Serikali ya kujengwa kwa viwanda katika maeneo haya.

2. Upatikanaji wa hati miliki kwa maeneo ya Dunga pamoja na Nyamanzi ni changamoto nyengine ambayo Kamati imeibaini, ambapo ilielezwa kuwa urasimu unaofanywa na baadhi ya taasisi za Serikali ikiwemo Wizara ya Ardhi inaonekana kuwa ni kikwazo juu ya jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na Wizara katika upatikanaji wa hati hizi.

3. Uwelewa mdogo wa wananchi juu ya kinachoendelea kufanyika katika eneo la uwekezaji Dunga.

   Kamati imebaini kuwa wananchi wengi ambao wanaishi karibu na maeneo hayo hawana utambuzi wa kinachoendelea kujengwa ndani ya eneo hilo.

4. Katika eneo linalotarajiwa kufanyika maonyesho ya kibiashara Nyamanzi, Kamati imepata wasiwasi mkubwa juu ya uvamizi unaoweza kufanywa na wananchi kutokana na ukubwa wa eneo hilo ambalo hadi sasa bado Serikali haijachukuwa hatua yoyote ya kulidhibiti eneo hilo.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kuzifanyia matengenezo barabara ziendazo katika maeneo ya miradi ya ujenzi wa viwanda kwa lengo la kuwavutia wawekezaji waweze kuyafikia maeneo hayo kwa urahisi. Aidha Kamati inaishauri Wizara kuweka miundombinu hii kuwa bora zaidi ili kuwahamasisha wawekezaji wengi kuweza kuwekeza katika maeneo hayo. Kamati inaipongeza Wizara ya Biashara kwa mashirikiano yake ya karibu na Wizara ya Mawasiliano kwa kuanza kuifanyia matengenezo barabara iendayo katika maeneo yanayotarajiwa kujengwa viwanda Dunga. Kamati inasisitiza kasi zaidi iongezeke katika kukamilisha matengenezo hayo.

2. kutokana na umuhimu wa maeneo haya, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuondosha urasimu uliopo hivi sasa na kuyapatia hati miliki maeneo yote ya uwekezaji, ambayo hadi sasa bado hayana hati miliki kwa lengo la kuyanusuru na kuondosha migogoro kati

ya Serikali na wananchi wanaoishi karibu na maeneo hayo hapo baadae.

3. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kutoa taarifa rasmi pamoja na elimu ya kutosha kwa wananchi wa eneo linalotarajiwa kujengwa viwanda Dunga juu ya miradi inayoendelea hivi sasa, hii itasaidia kuondosha malalamiko yanayoendelea kujitokeza siku hadi siku kutoka kwa wananchi dhidi ya Serikali yao.

4. Kamati inaishauri serikali kuchukua hatua za haraka za kulidhibiti eneo la uwekezaji Nyamanzi kwa lengo la kulinusuru na uvamizi, ambao hapo baadae unaweza kuzua migogoro mikubwa kati ya Serikali na wananchi wanaoishi karibu na eneo hilo.

5. Kamati pia inaishauri Wizara kuongeza kasi ya ufuatiliaji wa matokeo ya tafiti zilizokwishafanyika juu ya viwanda gani vinaweza kujengwa katika eneo la Pangatupu kwa lengo la kuepusha hasara kwa wawekezaji wetu hapo baadae.

6. Kamati inaipongeza Wizara ya Biashara pamoja na Mkoa wa kusini Unguja, Mkoa wa Kaskazini Unguja na Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa uamuzi wake wa kuyachaguwa maeneo hayo kuwa ni miongoni mwa maeneo ya uwekezaji, ambapo kufanikiwa kwa uwekezaji huu kutafungua fursa nyingi za ajira kwa vijana wetu.

## ZIARA KATIKA KIWANDA CHA MAJI - KINYIKANI PEMBA

Ujenzi wa kiwanda hiki umeanza tokea mwaka 2021 kwa gharama takribani dola laki nne za Kimarekani na kwa sasa kiwanda kimeanza uzalishaji wake.

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

Katika ziara yake hii, Kamati imebaini changamoto kadhaa ambazo zinaweza kuzorotesha uzalishaji kiwandani hapo. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:

1. Uchakavu wa miundombinu ya barabara ya kufikia kiwandani hapo, hasa

tukizingatia kiwanda hiki kipo nje kidogo ya mji. Ubovu huu wa miundombinu ya barabara unaweza kurudisha nyuma kasi ya maendeleo ya kiwanda hiki.

2. Changamoto nyengine iliyobainika ni ile ya kupanda na kushuka kwa kiwango cha umeme, kunapelekea hasara kubwa katika uzalishaji kiwandani hapo.

3. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati, kiwanda tayari kimeanza uzalishaji wake lakini hadi kamati inafika kiwandani hapo, Taasisi ya Viwango (ZBS) bado hawajatoa kibali cha bidhaa hii kuweza kuingia sokoni, hali inayotoa taswira mbaya hasa tukizingatia kwamba uzalishaji unaendelea kiwandani hapo siku hadi siku.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano, kuifanyia matengenezo barabara iendayo katika kiwanda hiki, ili kuweza kuibua fursa kwa wanunuzi wa bidhaa hii kuweza kufika kirahisi kiwandani hapo.

2. Kamati inaupongeza uongozi wa Kiwanda hiki kwa hatua ilizozichukuwa za kununua kifaa cha kuzibiti umeme (***stabilizer)*** ambayo kwa kiasi kikubwa imesaidia kupunguza tatizo la kupanda na kushuka kwa umeme kiwandani hapo. Hata hivyo, Kamati inaushauri uongozi huo kutafuta mbinu mbadala zitakazoweza kuondosha kabisa tatizo hili ili kiwanda kiweze kuepuka hasara ambayzo kwa sasa inakabiliana nazo.

3. Kamati inaipongeza sana Wizara ya Biashara kupitia Taasisi yake ya Viwango, kwa kukamilisha zoezi la upimaji wa sampuli za maji kiwandani hapo na kiwanda tayari kimepatiwa alama ya ubora kwa bidhaa inayoizalisha na bidhaa tayari

imeweza kuingia sokoni.

4. Kamati inachukuwa nafasi hii kutoa pongezi zake za dhati kwa uongozi wa kiwanda hiki, kwa maamuzi yake sahihi ya kuamua kuwekeza huduma hii muhimu kwa jamii kisiwani hapa. Kamati inaushauri uongozi huo kuongeza wigo wa kuwekeza viwanda zaidi vitakavyoweza kuzalisha bidhaa nyengine za vinywaji kama vile juisi za matunda mbalimbali hasa tukizingatia upatikanaji wa rasilimali zake zinapatikana kirahisi kisiwani hapa.

## ZIARA KATIKA KIWANDA CHA MWANI -CHAMANANGWE PEMBA

Kamati ilipata nafasi ya kukagua Mradi wa Ujenzi wa Kiwanda cha Mwani kilichopo Chamanangwe kisiwani Pemba, kwa lengo la kuangalia mendeleo ya mradi huu.

Mradi huu ulianza tarehe 27 Julai 2022 na hadi kukamilika kwake utagharimu jumla ya shilingi za kitanzania Bilioni 8.2, ukihusisha ujenzi wa uzio, jengo kubwa la kiwanda pamoja na ghala la kuhifadhia mwani.

Kamati inaipongeza sana Wizara ya Biashara pamoja na kikosi cha ulinzi KMKM, kwa hatua nzuri iliyofikiwa ya ujenzi huu, ambapo waliweza kuzitatua changamoto zote katika hatua ya awali kabisa na kwa muda huu ujenzi unaendelea vizuri na uko katika hali ya kuridhisha kabisa.

Kutokana na hali hii, kamati inaendelea kuwashauru Kikosi chetu cha KMKM pamoja na Wizara, kuendeleza mashirikiano yaliyopo ili kuhakikisha kuwa, Mradi huu unamalizika kwa wakati uliopangwa.

## ZIARA KATIKA UMOJA WA WAZALISHAJI WA ASALI MACHOMANE CHAKECHAKE – PEMBA

Lengo la kuanzishwa kwa Umoja huu ni kuwaunganisha wafugaji wa nyuki kisiwani Pemba kwa lengo la kuwawezsha kuzalisha asali kwa wingi, iliyo safi na yenye viwango.

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

1. Wafugaji kukosa elimu ya kutosha juu ya ufugaji wa nyuki kitaalamu, hali inayorudisha nyuma maendeleo ya wafugaji hao.

2. Changamoto nyengine iliyoelezwa ni ile ya kukosekana kwa Sera na Sheria

zinazowaongoza wazalishaji wa asali katika shughuli zao, hasa pale zinapotokezea changamoto, utatuzi wake unakuwa mgumu kwa sababu ya kukosa miongozo ya kisheria.

3. Uchakachuaji wa asali toka kwa wafugaji wa nyuki ni changamoto nyengine ambayo inashusha soko la bidhaa hii kisiwani Pemba. Baadhi ya wavunaji wa asali wanakosa uaminifu kwa kuichanganya asali na vitu vyengine jambo linaloishusha hadhi asali yetu.

4. Changamoto ya usafiri wa kuzifuata asali katika maeneo husika ni miongoni mwa changamoto zilizoelezwa.

5. Umoja unakosa ofisi ya uhakika ya kutelekezea majukumu yake. Ofisi iliyopo hivi sasa inaonekana kuwa na mgogoro kati ya Umoja uliopita na huu uliopo hivi sasa, jambo linalopunguza morali ya kiutendaji.

6. Aidha, vipimo vya kupimia ubora na usafi wa asali viliopo kituoni hapo ni hafifu, wanajumuiya hutumia uzoefu zaidi katika kupima asali kuliko vipimo hivyo.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Tasisi ya Viwango Zanzibar, kuwa karibu sana na wafugaji wa nyuki kwa lengo la kuwapatia taaluma yenye kufaa katika uzalishaji wao.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, kuharakisha uandaaji wa Sera na Sheria zitakazowaongoza wazalishaji wa asali katika shughuli zao ili wafugaji hawa waweze kupata miongozo sahihi katika kutatua changamoto zinazowakabili.

3. Kamati inaushauri Umoja wa Wazalishaji wa Asali kisiwani Pemba, kuzalisha

bidhaa hii katika hali ya ubora na yenye viwango. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara, kuwapatia elimu ya kutosha wazalishaji wa asali, juu ya kuzalisha bidhaa hii huku wakizingatia zaidi soko la nje ya nchi ambalo ni lenye tija na faida kubwa.

4. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kufanya utaratibu utakaowezesha wazalishaji wa asali kupata usafiri wa uhakika ambao watautumia katika harakati zao.

5. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kukaa pamoja na Umoja wa Wazalishaji wa asali uliopo na ule waliopita, kwa lengo la kujadili na kutatua mgogoro uliopo kuhusiana na ofisi.

6. Kamati inaishaurri Wizara, kuwapatia wazalishaji wa asali kituoni hapa elimu ya kutosha juu ya matumizi sahihi ya vipimo vya asali ili kuondokana na kutumia uzoefu zaidi katika kupima asali wakati wa mauzo.

7. Pamoja na yote hayo, Kamati inaupongeza Umoja wa Wazalishaji wa Asali - Machomane kisiwani Pemba kwa juhudi zake za kuhakikisha kuwa asali inayozalishwa inakidhi viwango na ubora unaotakiwa ili kulinda soko kisiwani hapa.

## ZIARA KATIKA KITUO CHA MAFUNZO YA KUSARIFU MAZAO YA KILIMO – KIZIMBANI UNGUJA.

Kamati ilipata nafasi ya kutembelea katika kituo cha kusarifu mazao ya kilimo Kizimbani Unguja *Namri* kwa lengo la kuangalia maendeleo ya wajasiriamali katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali ikiwa ni pamoja na tungule za kipaketi (tomato paste), sabuni za michi, ubuyu wa chokolati, sabuni za kuogea aina mbalimbali, dawa za kuoshea choo, dawa za kuoshea nywele (shampoo).

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

1. Wazalishaji katika kituo hiki wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa mitaji katika kuendeleza uzalishaji wa bidhaa zao. Maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati yalithibitisha mahitaji makubwa ya bidhaa zinazohitajika ambapo uzalishaji kwa sasa unakabiliwa na changamoto ya upungufu wa mitaji ili kufikia lengo la mahitaji hayo.
2. Wazalishaji katika kituo hiki wanakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa malighafi unaosababishwa na uhaba wa mitaji unaopelekea uzalishaji mdogo wa bidhaa kituoni hapo.
3. Alama za ubora bado ni changamoto kwa bidhaa zinazozalishwa.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kupitia SMIDA kuwapatia fursa za mikopo wajasiriamali hawa, kwa lengo la kuongeza uzalishaji kulingana na soko liliopo hivi sasa.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kupitia SMIDA, kuwapatia fursa za upatikanaji wa mitaji kwa lengo la kununulia malighafi zinazohitajika katika kikundi hicho, lengo ni kuongeza uzalishaji na kuweza kukidhi mahitaji ya soko liliopo.

3. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kupitia Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) kuengeza kasi mchakato wa upatikanaji wa alama za ubora kwa bidhaa zinazozalishwa ili lengo la uzalishaji wa bidhaa kituoni hapo liweze kufikiwa.

4. Kamati inaipongeza SMIDA kwa miongozo yao sahihi inayoitoa kwa kikundi hiki cha wajasiriamali juu ya mbinu bora za kuweza kujikwamua kiuchumi. Hata hivyo, Kamati inaishauri SMIDA kuendelea kutoa elimu zaidi kwa kikundi hiki kwa kuwaunganisha wajasiriramali hawa katika monyesho mbalimbali ya kibiashara, kitaifa na kimataifa ili waweze kutanua wigo katika kuzitangaza bidhaa zao, kukuza uzalishaji na ubora wa bidhaa wanazozizalisha.

**TAASISI NA MASHIRIKA YALIYOMO NDANI YA WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA.**

1. **WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI UNGUJA NA PEMBA**

Kamati ilifika katika ofisi za Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali Zanzibar kwa lengo la kuangalia utekelezaji wa majukumu ya kila siku katika Taasisi hii.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA MALI - UNGUJA NA PEMBA**

Katika ziara yake hii, Kamati ilibaini changamoto kadhaa ambazo zinachangia kukwamisha utekelezaji wa majukumu ya Taasisi hii siku hadi siku. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na: -

1. Tatizo la usafiri, ni tatizo kubwa katika ofisi za Wakala ambapo Kamati imebaini kuwa, ofisi zote Unguja na Pemba zinakabiliwa na tatizo hili.

2. Ufinyu wa ofisi ni changamoto inayokwaza utekelezaji wa majukumu ya taasisi hii muhimu hasa tukizingatia huduma zinazotolea na unyeti wa taasisi hii.

3. Vile vile, ofisi ya Pemba inakabiliwa na changamoto ya idadi ndogo ya wafanyakazi. Kwa mujibu wa taarifa iliyopokelewa, ni wafanyakazi tisa tu ndio waliopo kwa sasa ambao hawakidhi haja na matakwa ya kiutendaji.

**MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI**

1. Kamati inaishauri Wizara kuchukuwa hatua za makusudi kuhakikisha tatizo la usafiri katika taasisi hii linapatiwa ufumbuzi wa kudumu.
2. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kujenga majengo ya kudumu kwa ajili ya ofisi za taasisi zake, lengo ni kuboresha mazingira mazuri ya kiutendaji katika taasisi hii.
3. Kamati inaishauri Serikali kuipatia ofisi hii wafanyakazi wa kutosha watakaoweza kutekeleza majukumu ya taasisi kwa ufanisi zaidi.

4. Pamoja na yote hayo Kamati inaipongeza Wakala kwa juhudi zake katika utekelezaji wake mzuri wa majukumu kwa kuweza kukiuka malengo ya ukusanyaji wa mapato. Kamati inaishauri taasisi hii kuvilinda vianzio vyote vya mapato ili kuongeza kasi ya ukusanyaji wa mapato hayo.

5. Kamati inaipongeza taasisi hii kwa utekelezaji mzuri wa majukumu yake katika mazingira magumu. Aidha, Kamati inaishauri taasisi hii kuondokana kabisa na masuala ya urasimu katika kuwapatia wananchi huduma zilizo bora.

6. Kamati inaishauri taasisi kuendeleza mashirikiano kati yake na taasisi nyengine kama vile ZRB kwa lengo la kufanikisha azma ya Serikali ya kuogeza kiwango cha ukusanyaji mapato siku hadi siku.

7. Kamati pia inaishauri taasisi hii kuendelea kutoa elimu kwa jamii juu ya uwepo wa taasisi hii ili waweze kuitumia katika upatikanaji wa huduma zinazotolewa kwa maendeleo yao na taifa kwa ujumla.

2. WAKALA WA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO VIDOGO, VIDOGO NA VYA KATI (SMIDA)

Wakala wa Maendeleo ya Viwanda vidogo vidogo, vidogo na vya kati (smida) kisiwani Pemba inafanya kazi chini ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda. Ofisi hii inafanya kazi kwa mujibu wa sheria Namba 2 ya mwaka 2018. Kazi kubwa ya Ofisi hii ni kushirikiana na wajasiriamali kufanikisha shughuli zao hasa za viwanda vidogovidogo, vidogo na vya kati. Kwa upande wa Pemba Ofisi hii inafanya kazi katika maeneo mawili makubwa Wete na Chake Chake Pujini.

## CHANGAMOTO ZA WAKALA WA MAENDELEO YA VIWANDA VIDOGO VIDOGO, VIDOGO NA VYA KATI (SMIDA)

Katika ziara yake hii, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo: -

1. Kamati ilibaini changamoto ya ufinyu wa ofisi. Ofisi inayotumiwa na taasisi hii muhimu kwa maendeleo ya wajasiriamali wetu haiko katika hali ya kuridhisha.

2. Kukosekana kwa usafiri katika taasisi hii ni changamoto nyengine iliyoelezwa mbele ya Kamati. Maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati yalibainisha kwamba kwa sasa usafiri unaotumiwa na ofisi katika utekelezaji wa shughuli zake ni usafiri wa mtu binafsi (Mratibu) ambao kwa kweli si rafiki kabisa.

3. Kamati pia ilibaini uwepo wa mashine ya kuchakata matunda ambayo imekaa kwa kipindi kirefu sasa bila ya kufanyiwa kazi yoyote. Tukumbuke kwamba mashine hii iligharimu fedha nyingi sana katika kupatikana kwake na kukaa bila ya kutumika inaweza kuharibika na kuitia hasara kubwa Serikali.

4. Uhaba wa wafanyakazi katika taasisi hii ya SMIDA ni changamoto nyengine ambayo Kamati iliibaini. Jumla ya wafanyakazi watano tu (5) ndio waliopo katika taasisi hii wakiwemo afisa Mipango, Mratibu, Makarani wawili pamoja na mlinzi.

5. Ukosefu wa kituo cha kufanyia shughuli za uzalishaji wa pamoja kwa wajasiriamali ni miongoni mwa changamoto iliyoelezwa kwa Kamati. Ilielezwa kwamba katika visiwa vyetu wapo wajasiriamali wengi ambao wanakosa sehemu maalum ya pamoja ya kufanyia shughuli zao jambo linalorudisha nyuma maendeleo yao siku hadi siku.

6. Kamati pia ilibaini changamoto ya mtaji mdogo kwa wajasiriamali wetu, hali inayopelekea kusuasua kwa uzalishaji wa bidhaa zao wanazozizalisha.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inachukuwa nafasi hii kuishauri Wizara ya Biashara kuchukuwa hatua za makusudi za kutafutia ofisi iliyo rafiki zaidi kwa kuzingatia shughuli muhimu zinazofanywa na taasisi hii.

2. Usafiri katika taasisi hii ni muhimu kwa maendeleo yake na taifa kwa ujumla, hivyo Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kutafuta usafiri wa kudumu ili kurahisisha maendeleo ya taasisi hii.

3. Kamati inaishauri SMIDA kutafuta njia muafaka ambazo zitaifanya mashine iliyopo katika ofisi za SMIDA Pemba, kufanyakazi japo kwa kuwakodisha wajasiriamali wenye uwezo.

4. Sote ni mashahidi kuwa, wafanyakazi katika taasisi yoyote ile ndio kiungo cha mafanikio katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku, kinyume chake ni kuzorota kwa utekelezaji huo. Kwa muktadha huu, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Utumishi wa Umma, kuongeza idadi ya wafanyakazi kwa mujibu wa kada zinazohitajika kwa lengo la kupeleka mbele gurudumu la maendeleo katika taasisi hii muhimu.

5. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kujenga kituo cha kufanyia shughuli za uzalishaji wa pamoja kwa wajasiriamali waliopo nchini kwa lengo la kuboresha uzalishaji wa bidhaa zao.

6. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kupitia SMIDA kutoa elimu zaidi kwa wajasiriamali juu ya fursa ziliopo hivi sasa kama vile mikopo kutoka mabenki yetu nchini kwa lengo la kujiimarisha zaidi kiuchumi.

7. Pamoja na changamoto hizo, Kamati inaipongeza Ofisi ya SMIDA kisiwani Pemba kwa kufanyakazi katika mazingira magumu na kuweza kufikia malengo iliyojipangia.

8. Aidha Kamati inaishauri SMIDA kuendeleza na kudumisha mashirikiano kati yake na Wizara ya Uwekezaji kwa lengo la kuondosha urasimu ili kurahisisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya wajasiriamali wetu.

## 3. SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC)

Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) lilianzishwa kwa Legal Notice No.39 ya mwaka 1968. Mnamo mwaka 2011 Serikali ilifanya mapitio ya mfumo mzima wa sekta ya karafuu na muundo wa utekelezaji na majukumu ya Shirika yaliyopelekea kuundwa kwa Sheria ya Shirika la Biashara la Taifa Na.11 ya 2011. Mapitio hayo ya muundo wa Shirika yamepelekea kuundwa kwa mfuko wa Maendeleo ya Karafuu kwa Sheria Nam. 2 mwaka 2014 (Clove Development Act No.2 of 2014).

Kutokana na mwenendo wa Shirika kwa sasa pamoja na umuhimu wa zao la karafuu kwa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu, Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kwa makusudi iliamua kufanya ziara katika Shirika hili kwa Unguja Pemba kwa lengo la kujionea mwenendo mzima wa biashara na utendaji wa Shirika lenyewe.

Kamati ilifanikiwa kukagua baadhi ya Miradi ya Shirika ikiwa ni pamoja na: -

a) Mradi wa Ujenzi wa Maghala ya Kuhifadhia Karafuu -Madungu;
b) Mashine za kupimia unyevunyevu wa karafuu – Pemba;
c) Vituo vya kununulia karafuu Mkoani, Wete;
d) Shamba la Mikaratusi Mamoja - Tumbe;
e) Kiwanda cha Mafuta ya Majani ya Karafuu - Mtambwe.

MRADI WA UJENZI WA MAGHALA YA KUHIFADHIA KARAFUU - MADUNGU,

Mradi huu ujenzi wake ulianza mwaka wa fedha 2018/2019 unaohusisha maghala matatu, jengo la uwekezaji, eneo la maduka, jengo la Benki, kituo cha manunuzi ya karafuu na maeneo ya maegesho ya magari. Aidha, mradi ulikisiwa kugharimu kiasi cha fedha za kitanzania bilioni 7, 246,300,328.95, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 6,923,355,649 ni kwa ajili ya ujenzi wa majengo hayo.

Kamati ilipotembelea katika eneo la mradi ilibaini changamoto zifuatazo:

1. Upatikanaji wa fedha ilikuwa ni changamoto kubwa iliyopelekea kusimama kwa ujenzi huu takriban kwa kipindi cha mwaka mzima. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa mbele ya Kamati, Ujenzi wa mradi huu ulisimama tokea mwezi wa Novemba 2020 hadi mwezi wa Disemba 2021 ambapo Shirika la ZSTC lilishindwa kumlipa Mkandarasi fedha kwa wakati kama mkataba unavyoelekeza.

2. Kutokana na changamoto ya kukosekana kwa fedha kulikosababisha kusimama kwa shughuli za ujenzi wa mradi huu kwa muda mrefu, Kamati inaamini kuwa ujenzi huu hauwezi kumalizika kwa wakati jambo ambalo liinarudisha nyuma kasi ya maendeleo ya Shirika hili kutokana na kuongezeka kwa gharama ya vifaa vya ujenzi.

3. Kamati imeelezwa changamoto ya kuwepo kwa sintofahamu baina ya Mkandarasi wa Ujenzi na Mshauri Elekezi wa Mradi, iliyosababishwa na

kuchelewa kwa kuingia kwa fedha kulikopelekea kupungua kwa kasi ya maendeleo ya mradi huu.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Pamoja na changamoto hizo Kamati inachukuwa nafasi hii kuipongeza Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kupitia Shirika Lake la ZSTC kwa maamuzi yake sahihi ya kujenga maghala ya kuhifadhia karafuu ambayo yatasaidia katika utunzaji sahihi wa karafuu zetu ili ziweze kukidhi viwango vinavyohitajika kimataifa.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuandaa bajeti ya kutosha kuhusiana na miradi kama hii ya maendeleo. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuunga ubia na taasisi mbalimbali za kifedha kwa lengo la kutekeleza miradi kama hii na kuiwezesha miradi hii kumalizika kwa wakati.

3. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuongeza kasi ya usimamizi wa Mradi huu ili kuhakikisha kwamba mradi unamalizka kwa wakati uliopangwa na thamani ya fedha iliyotumika inaonekana.

4. Kamati inaipongeza Wizara ya Biashara kwa maamuzi yake sahihi ya kukutana na Mkandarasi pamoja na Mshauri Elekezi wa Mradi, kwa lengo la kuitatua changamoto iliyopo hivi sasa na kuongeza kasi ya ujenzi ili maghala yaweze kumalizika na kuanza matumizi.

5. Aidha, Kamati inamini kwamba, Kumalizika na kuanza matumizi kwa Maghala haya, ndio muarubaini wa tatizo la upungufu mkubwa wa chakula kisiwani Pemba, hasa tukizingatia kwamba, baadhi ya maghala haya, Wizara ina lengo la kuyakodisha kwa wafanya biashara ambao wataweza kuyatumia katika kuhifadhia chakula.

6. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuhakikisha kwamba Mshauri Elekezi anaonekana katika eneo la mradi muda wote ili

kuepusha ubabaishaji unaoweza kufanyika ambapo athari zake zitaweza kuifanya thamani ya fedha itakayotumika katika mradi huu isionekane.

7. Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kumsimamia Mkandarasi wa Ujenzi huu kwa karibu sana, ili kuondosha changamoto ndogondogo zinazojitokeza kwa lengo la kuupeleka mbele Mradi huu.

8. Katika kuhakikisha Mradi huu unakamilika kwa wakati, Kamati pia inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kutumia vikao vyake vya ndani katika kutatua changamoto zote zinazojitokeza katika hatua za awali kabisa.

9. Kamati inaishauri Wizara inapotekeleza miradi yake lazima ijiridhishe juu ya uwezo walionao wakandarasi wetu katika kutekeleza miradi hiyo kabla ya kuwapa malipo yao ***'cerificate'*** Hii itasaidia kuepusha matatizo ambayo yanaweza kujitokeza kabla ya kumalizika kwa miradi yetu. Kamati imebaini kwamba, mara nyingi wakandarasi wetu hujaribu kudanganya juu ya uwezo walionao katika nyanja tofauti kama vile fedha na wataalamu, na hatimae kushindwa kuikamilisha miradi waliyopangiwa kwa wakati.

## ZIARA YA KUKAGUA MASHINE YA KUPIMIA UNYEVUNYEVU WA KARAFUU.

Kamati pia ilipata nafasi ya kufika katika kituo cha kununulia karafuu Madungu Chakechake na kujionea hali halisi ya mashine zinazotumika katika kupimia unyevunyevu. Katika ziara yake hii Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:

## CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KATIKA ZIARA HII

Katika ziara hizo Kamati ilibaini changamoto zifuatazo: -

1. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati, Kamati ilibaini uhaba wa mashine za kupimia unyevu wa karafuu katika vituo vingi vya kununulia karafuu. Aidha Kamati ilielezwa kuwa ni mashine nne tu ziliopo kwa sasa na katika kituo hiki ni mashine moja iliyopo na kufanya kazi.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendelero ya Viwanda kuchukuwa hatua za makusudi kuhakikisha kuwa inaongeza idadi ya mashine za kupimia unyevunyevu wa karafuu katika vituo vyote vya kununulia karafuu kisiwani Pemba na Unguja kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kuhakikisha kuwa karafuu zinazonunuliwa ziko katika hali nzuri.

2. Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua yake ya awali ya kutafuta mashine hizi kwa lengo la kuwasaidia wafayabiashara wetu pamoja na wafanyakazi wanaofanya kazi katika vituo hivi. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuendeleza juhudi zake ilizozianza kwa kuongeza mashine nyengine kwa lengo la kuongeza ufanisi wa kiutendaji na kuondoa kabisa malalamiko kutoka kwa wakulima.

## KITUO CHA KUNUNULIA KARAFUU WETE NA MKOANI.

Kamati ilipata nafasi ya kufanya ziara katika vituo vya kununulia karafuu Wete na Mkoani Pemba kwa lengo la kujionea hali halisi ya mauzo kwa bidhaa hii muhimu kwa maendeleo ya taifa letu. Vituo ambavyo, kwa njia moja au nyengine vinasaidia sana katika kutoa huduma ya ununuzi wa karafuu toka kwa wakulima, ambapo kwa sasa vituo vipo katika hali nzuri katika kutoa huduma hizo bila ya usumbufu wowote.

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HIZI

Kamati katika ziara yake hii, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:

1. Katika Kituo cha kuuuzia karafuu Wete, wakulima wa karafuu walisikika wakililalamikia Shirika juu ya kukosekana kwa daraja lakwanza kwa karafuu zao.

2. Kamati pia ilibaini changamoto ya mifumo ya kibenki kuwakwaza wakulima wakati wa malipo kwa mauzo ya karafuu zao. Malipo yanaonekana kuchelewa kuwafikia kunakosababishwa na tatizo la mifumo ya kimtandao.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kuendelea kutoa elimu kwa wakulima wa karafuu juu ya mbinu bora zitakazosaidia karafuu zao kufikia daraja la kwanza.

2. Kamati inaishauri Wizara kuendelea kuwa karibu na watoa huduma wa kibenki ili kuondokana na tatizo la malipo kutowafikia wakulima kwa wakati.

3. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuhakikisha kwamba vituo vyote vya mauzo ya karafuu vinafuata kanuni na taratibu za mauzo ziliopo kwa lengo la kuepusha migogoro kati ya Shirika na wakulima wa karafuu.

4. Kamati inaipongeza Wizara ya Biashara kwa hatua zake ilizozichukuwa za kuhakikisha kuwa mashine za kupimia unyevu wa karafuu zinaendelea kufanya kazi katika vituo vyote vya mauzo. Kamati inaendelea kuishauri Wizara hii kupitia Shirika la Biashara kuzitunza mashine hizo ili ziweze kutumika kwa muda mrefu hasa tukizingatia kwamba mashine hizi ziligharimu fedha nyingi.

5. Kamati inaipongeza Wizara ya Biashara kwa hatua nzuri iliyofikia ya kuongeza idadi ya mashine za kuchekechea karafuu, toka mashine 12 hadi kufikia 20. Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda,

kuzisambaza mashine hizi katika vituo vyote kisiwani Pemba, ili zoezi la uuzaji na ununuzi wa karafuu liweze kutekelezeka bila ya usumbufu na Wizara iweze kukwepa ile hasara itokanayo na wakulima wasio waaminifu, wanaojaribu kuzichanganya karafuu zao na vitu vyengine ambavyo vinaipunguzia karafuu yetu kiwango stahiki wakati wa mauzo nje ya nchi.

6. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuwapatia elimu ya kutosha wauzaji wa karafuu, juu ya matumizi mbadala ya unga unaopatikana baada ya karafuu zao kuchekechwa. Unga huu ni rasilimali muhimu ambayo inaweza kutumika katika viwanda vidogovidogo viliopo nchini.

7. Kamati inaipongeza Wizara ya Biashara kwa kuwa na wafanyakazi wa kutosha wa kupima unyevu wa karafuu, hali inayopelekea utekelezaji mzuri wa majukumu yao vituoni. Wizara iendelee kuwaenzi wafanyakazi hao ili waendelee kulitumikia taifa lao kwa moyo mmoja.

## SHAMBA LA MIKARATUSI- MAMOJA TUMBE (ZSTC)

Shamba la Mikaratusi Mamoja ni shamba la Serikali liliopo chini ya Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) lenye ukubwa wa eka 45.0 sawa na hekta 18. Moja kati ya majukumu ya msingi ya Shirika la Biashara la Taifa (ZSTC) ni kutayarisha mashamba ya Mikaratusi kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mafuta ya malighafi hii hadi kufikia tani 2000 kwa mwaka.

Kamati ilipata nafasi ya kukagua shamba la mikaratusi Mamoja kisiwani Pemba kwa lengo la kujionea hali halisi ya uzalishaji wake. Katika ziara yake hii, Kamati ilibaini changamoto kadhaa zikiwemo hizi zifuatazo:

1. Baadhi ya wananchi walidai kwamba wameharibiwa vipando vyao wakati wa zoezi la matayarisho ya shamba hili, hali iliyozua mgogoro kati ya wananchi hao na watendaji wa ZSTC.

2. Maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati yalithibitisha uwepo wa mwamba katika eneo la shamba hili. Karibu ekari kumi za eneo hili zimeathirika na hali hii

ambapo Mikaratusi ilishindikana kupandwa katika eneo hilo.

3. Changamoto nyengine iliyoelezwa mbele ya Kamati ni ile ya gharama inayotokana na kusafirisha majani ya mikaratusi kutoka shambani hadi kiwandani.

4. Upatikanaji wa hati miliki wa shamba hili umekuwa ni kilio cha muda mrefu ambapo maelezo yaliyopokelewa mbele ya Kamati yalithibitisha kwamba, vikwazo vilivyozuia upatikanaji wa hati hiyo tayari vimetatuliwa na eneo tayari limeshapimwa lakini hati hiyo hadi sasa bado haijapatikana.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inalipongeza Shirika kwa hatua ilizozichukuwa za kutatua mgororo ulioibuka kati yake na wananchi waliodai kukatiwa vipando vyao wakati wa matayarisho ya shamba kwa njia za usalama na amani.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kupitia Shirika la Biashara la Taifa kutafuta mbinu mbadala itakayosaidia kulitumia eneo lililoathirika na mwamba ambapo hapo awali lilishindikana kupandwa malighafi hiyo.

3. Kamati inalipongeza Shirika kwa hatua ya utatuzi wa changamoto ya gharama ya kusafirishia majani ya mikaratusi toka shambani hadi kiwandani ambapo ilielezwa kwamba, maandalizi ya kujenga kinu cha kukamulia mafuta ya Mkaratusi shambani hapo yameshaanza na yapo katika hatua nzuri kabisa. Hivyo ni vyema kuongeza kasi zaidi kwa lengo la kukamilisha ujenzi kwa wakati uliopangwa

4. Hivyo Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kupitia Shirika hili kuongeza kasi ya ufuatiliaji wa upatikanaji wa hati miliki kwa shamba hili la Mamoja kwa lengo la

kuepusha migogoro hapo baadae.

**5.** Pamoja na hayo yote Kamati imeridhika na maendeleo ya shamba hili na tunalishauri Shirika kuendeleza zoezi la upandaji wa mikaratusi kwa lengo la kupata malighafi zaidi kwa ajili ya viwanda vyetu. Aidha tunalipongeza Shirika kwa hatua nzuri ya uzalishaji na uoteshaji wa Mikaratusi ndani ya shamba hili, hali inayotoa sura nzuri ya kufikiwa malengo ya Wizara hii na taifa kwa ujumla.

## KIWANDA CHA MAFUTA YA MAJANI YA MIKARAFUU- MTAMBWE

Shirika la Taifa la Biashara Zanzibar (ZSTC) liliingia makubaliano na Kampuni ya ENDESO kwa lengo na kukubaliana kuzalisha mafuta ya majani ya mikarafuu, ambapo Kampuni ilianzisha viwanda katika maeneo tafauti kisiwani Pemba ikiwa ni pamoja na hiki cha Mtambwe. Katika kulifanikisha hili jumuiya ya Wazalishaji wa Mafuta ya Majani ya Mikarafuu iliundwa ambayo inajulikana kama "***Umoja wa Wazalishaji wa Mafuta ya Majani ya Mikarafuu"*** Ukiwa na lengo la kusaidia ajira kwa vijana***,*** kwa mujibu wa maelezo yaliyopokelewa mbele ya Kamati karibu vujana 200 wameajiriwa katika viwanda hivi.

## CHANGAMAOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

1. Umoja wa Wazalishaji wa mafuta walilalamikia Shirika la ZSTC kwa kuchukuwa dola moja ya mapato yatokanayo na mauzo ya rasilimali hii. Kampuni ya ENDESO imeeleza kuwa inatumia gharama kubwa katika uzalishaji wa mafuta kiwandani hapo hali inayopelekea hasara kubwa kiwandani hapo.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kutokana na malalamiko ya wanajumuiya ya wazalishaji wa mafuta juu ya dola moja inayoingia katika Shirika la ZSTC Kamati inaishauri Wizara ya Biashara kupitia Sirika hili, kukaa pamoja na wanajumuiya hawa na kutafuta mbinu za kutatua kadhia hii kwa njia za usalama na amani. Sheria na kanuni ziliopo ni vyema zikapitiwa upya kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu yaliyopo.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kutoa elimu zaidi kwa jumuiya za wazalishaji mafuta kwa lengo la kuwajengea uelewa zaidi katika kutekeleza kazi zao.

## WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inaundwa na Idara na taasisi mbali mbali ambazo kwa pamoja zina lenga kutoa huduma kwa wananchi wote ndani ya visiwa hivi bila ubaguzi wowote.

## IDARA ZA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

1. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
2. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
3. Idara ya Utalii
4. Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale
5. Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe
6. Afisi ya Afsa Mdhamini - Pemba.

## TAASISI ZA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

1. Kamisheni ya Utalii.

## PROGRAMU KUU ZA WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE

Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inatekeleza majukumu yake ya kila siku kupitia Programu kuu tano (5) kama zifuatazo: -

1. Programu Kuu ya Maendeleo ya Makumbusho, Mambo ya kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe;

2. Programu Kuu ya Kusimamia Maendeleo ya Utalii;

3. Programu Kuu ya Utangazaji na Uhamasishaji wa Utalii;

4. Programu Kuu ya Kuratibu na Kusimamia Maendeleo ya Utalii

5. Programu Kuu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Utalii.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA MAKUMBUSHO, MAMBO YA KALE NA UHIFADHI WA MJI MKONGWE

Lengo kuu la Programu kuu hii ni kuwa na Mji Mkongwe na Maeneo ya Kihistoria yaliyohifadhiwa, kuimarishwa na kuendelezwa kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadae ambapo matokeo ya muda mrefu ni kuyahifadhi, kuyalinda, kiyatangaza, na kuyaendeleza maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini pamoja na uhifadhi wa Mji Mkongwe ili kubakia kuwa urithi wa kitaifa, kikanda na kimataifa.

Programu Kuu hii inajumuisha programu ndogo mbili ambazo ni: -

i) Programu ndogo ya Uendelezaji wa Makumbusho, Mambo ya Kale na Uhifadhi wa Mji Mkongwe;

**ii)** Programu ndogo ya Uimarishaji wa Kumbukumbu na Nyaraka.

## ZIARA ZA KAMATI KUANGALIA MAENDELEO YA PROGRAMU HII.

Kamati katika kazi zake ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali kwa lengo la kukagua Miradi ya maendeleo na maeneo Mmbalimbali ya kihistoria kwa lengo la kuona maendeleo yake pamoja na tija inayopatikana kupitia maeneo hayo. Kupitia programu hizi, Kamati ilifanya ziara katika maeneo yafuatayo: -

i) Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe;
ii) Makumbusho ya Amani na Makumbusho ya Viumbe Hai;
iii) Eneo la kihistoria la Maruhubi;
iv) Eneo la kihistoria la Kasri la Kibweni, Kasri la Selme- Bububu;
v) Eneo la kihistoria Mangapwani;
vi) Ukarabati wa ujenzi - Pango la Watoro;
vii) Ukakarabati wa Ujenzi -Pango la Kijiji Makangale;

viii) Eneo la kihistoria Chwaka Tumbe;

ix) Eneo la Kihistoria Rasi Mkumbuu;

x) Jamati la Wahindi, Msikiti pamoja na Makaburi ya Mabohora- Kengeja;

**xi)** Maeneo ya kihistoria ya kimaumbile - Panga Samaki, Pango Ulingo, Majabali ya Kachunge na Katenga, Mbuyu wa Vasgodagama, kisiwa cha ndege, Gati ya Zamani na Mto Furaha.

## ZIARA KATIKA MAMLAKA YA HIFADHI NA UENDELEZAJI WA MJI MKONGWE.

Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji wa Mji Mkongwe ina jukumu la kuhakikisha urithi wa kihistoria wa majengo, utamaduni wa asili, mandhari na vivutio vyengine vinabakia katika hali yake kwa faida ya sasa na vizazi vijavyo sambamba na kudumisha hadhi ya mji wetu duniani.

## CHANGAMOTO ZA MAMLAKA YA MJI MKONGWE.

1. Kamati ilielezwa changamoto ya uingiaji wa vyombo vya moto katika Mji Mkongwe kinyume na utaratibu sambamba na uegeshaji wa vyombo hivyo katika maeneo yasiyoruhusiwa hali inayoondosha haiba ya mji wetu huu.

2. Kamati ilielezwa pia changamoto ya uhaba wa mafundi wenye ujuzi ambao kwa sasa ni mafundi watano tu (5) waliopo na wengine tayari wameshastaafu.

3. Upatikanaji wa vifaa vya asili kwa ajili ya uhifadhi ni changamoto nyengine ambayo iliielezwa mbele ya Kamati. Miongoni mwa vifaa hivyo ni pamoja na boriti, mawe, udongo na chokaa.

4. Kupanda kwa gharama za vifaa vya asili kama vile milango ya nakshi na hii ni kutokana na thamani yake kwa jamii.

5. Kamati imebaini changamoto ya baadhi ya majengo ya Mji Mkongwe kuwa hayapo katika hali nzuri jambo linaloondosha haiba ya Mji Mkongwe na kuendelea kuiondosha sura ya Mji ambao ndio urithi wa dunia.

MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuandaa utaratibu mzuri wa uingiaji wa vyombo vya moto pamoja na maegesho ya magari kwa lengo la kuepusha usumbufu unaoendelea kuwapata watumiaji wa barabara katika maeneo yote ya Mji Mkongwe.

2. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara aya Utalii na Mambo ya Kale kuchukuwa hatua za makusudi kutafuta mafundi wa kutosha wenye ujuzi ambao wataweza kufanikisha ujenzi wa jengo hili.

3. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuhakikisha kwamba vifaa vya asili vinavyohitajika katika ujenzi wa jengo hili la Beit -Aljaib vinapatikana muda wote pamoja na kwamba upatikanaji wake ni wa tabu.

4. Pamoja na kuwa milango ya asili ni gharama, Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuhakikisha kuwa milango hiyo inaendelea kutumika katika majengo ya nyumba za Mji Mkongwe kwa lengo la kuudumisha na kuuendeleza urithi wa utamaduni kwa vizazi vijavyo na dunia kwa ujumla.

5. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuunga ubia na watu binafsi na mashirika mbalimbali ya kifedha kwa kuyafanyia ukarabati majengo yote ya Mji Mkongwe ambayo hayapo katika hali nzuri. Aidha, Wizara iwe karibu sana na wawekezaji wenye nia ya kuyafanyia ukarabati majengo ambayo hayapo katika hali nzuri kwa lengo la kuyarudisha katika haiba yake ya asili.

6. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuuhimiza uongozi wa Oman juu ya kuharakisha kuanza kwa ukarabati wa jengo hili ili kulinusuru na

athari nyengine ambazo zinaweza kutokezea.

## ZIARA KATIKA MAKUMBUSHO YA AMANI NA MAKUMBUSHO YA VIUMBE HAI (MNAZI MMOJA)

Kamati ilifanya ziara katika Makumbusho ya Amani na Makumbusho ya Viumbe Hai na kuelezwa kuwa sehemu hiyo hapo awali ilikua ikitumika kwa kufanyia maonyesho ya historia ya Zanzibar pamoja na kuhifadhia wanyama aina mbali mbali ambao kwa sasa wametoweka ila juhudi zinafanyika za kukarabati eneo hilo na kurudisha wanyama na vitu vyote vilivyokuwepo hapo awali.

## CHANGAMOTO ZA MAKUMBUSHO YA AMANI NA MAKUMBUSHO YA VIUMBE -HAI

Katika Makumbusho ya Amani na Makumbusho ya Viumbe hai Kamati ilielezwa changamoto zifuatazo: -

1. Kuongezeka kwa upeo wa mradi (scope)ndani ya utekelezaji wa mradi uliosababishwa kuongezwa ukubwa kati ya vyumba vilivyopo katika makumbusho hayo, ambapo hapo awali vyumba hivyo vilikuwa ni kidogo mno.

2. Sakafu iliyopo katika makumbusho hayo inatarajiwa kuparwa kwa kiwango kikubwa kwa lengo la kuweka uimara, hali inayohitaji umakini.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Aidha, Kamati inatoa pongezi zake za dhati kwa Wizara ya Utalii kwa hatua iliyofikiwa ya kukamilisha ukarabati wa Makumbusho ya Viumbe hai na Amani.
2. Kamati inashauri Wizara ya Utalii kufanya upembuzi yakinifu kabla ya kuanza kwa mradi ili mahitaji yote yanayohitajika yaweze kupatikana kwa wakati.

## ZIARA KATIKA ENEO LA KIHISTORIA LA MARUHUBI

Eneo la kihistoria Maruhubi lilijengwa na Sultan Bar-ghash kwa lengo la kustarehe yeye mwenyewe pamoja na Masuria wake. Jengo lilihusisha mabwawa ya kuogelea '***swimming pool***' pamoja na Mahamamu kadhaa.

Katika ziara hii Kamati ilibaini changamoto kadhaa. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na hizi zifuatazo:

## CHNGAMOTO KATIKA ENEO LA KIHISTORIA MARUHUBI

1. Kamati ilibaini changamoto ya Uchakavu wa jengo ambao unaondosha haiba nzuri ya eneo hili. Jengo linaonekana kupigwa na maji ya mvua zinazonyesha na kuotesha kwa miti mingi ndani yake.

2. Kamati imejionea kwa macho yake changamoto ya kuoza kwa boriti zilizotumika kujenga jengo hilo, hali inayopelekea kuhatarisha maisha ya jengo hilo ambalo ni kivutio kizuri kwa wageni wanaofika hapo.

3. Kamati imesikitishwa na uhaba mkubwa wa wafanyakazi uliopo katika eneo hili. Wafanyakazi watatu tu ndio waliopo katika eneo hili hali inayowapa ugumu wafanyakazi hao katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

4. Kamati pia ilijionea uharibifu unaofanywa na wananchi wanaolitumia eneo hili kwa mila na utamaduni. Maeneo kadhaa yameenea damu ambayo inaonekana wazi kuwa wananchi hufanya vichinjo na kuacha mabaki hayo ndani ya jengo hilo. Aidha wananchi hao hujaribu kuchimba mashimo ambayo huharibu mazingira ya eneo hilo na kuodosha haiba nzuri iliyopo.

5. Kukosekana kwa ofisi katika eneo hilo ni changamoto nyengine ambayo hupelekea walinzi wanaokuwepo kukosa hata sehemu ya kukaa na kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

6. Kamati pia ilielezwa changamoto ya kutoweka kwa vikundi jamii ambavyo vilisaidia katika kuimarisha ulinzi katika eneo hili.

7. Kamati imebaini changamoto ya kukosekana kwa hati miliki ya eneo hili hali inayopelekea wananchi kulivamia eneo kwa shughuli zao za kijamii ikiwemo ile ya kilimo.

8. Kamati ilielezwa changamoto ya mipaka baina ya Shirika la Bandari na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale, changamoto ambayo inaweza kuathari na kuleta migogoro hapo baadae.

9. Kamati imebaini changamoto ya kukosekana kwa choo (maliwato) katika eneo hili, hali inayowapa wakati mgumu walinzi na wageni wanaofika katika eneo hili.

10. Kamati imebaini changamoto ya miundombinu ya barabara isiyoridhisha iendayo katika eneo hili la kihistoria.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kutenga bajeti maalumu kwa lengo la kulifanyia ukarabati na kuliimarisha jengo hili ili kuongeza vivutio vya utalii na watalii nchini.

2. Kamati inaishauri Wizara kuongeza idadi ya wafanyakazi katika eneo hili muhimu la kihistoria kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku.

3. Kamati inaishauri Wizara kuandaa utaratibu, miongozo na kanuni maalum zitakazowaongoza wananchi wote wanaofika katika eneo hili kwa lengo la kufanya mambo ya kijadi na kuhakikisha kwamba wanatunza mazingira ya ndani na nje ya eneo hili.

4. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Utalii kuwawekea mazingira rafiki wafanyakazi wa eneo hili kwa kuwajengea ofisi watakayoweza kuitumia katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

5. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kuandaa utaratibu mzuri wa kuvirejesha vikundi vya kijamii ambavyo vilikuwa vikitumika katika harakati za ulinzi wa eneo hili, lengo ni kuimarisha ulinzi kwa wageni wanaoingia katika eneo hili.

6. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuharakisha upatikanaji wa hati miliki wa eneo hili. Aidha, Kamati inalishauri Wizara ya Utalii kukaa pamoja na Shirika la Bandari kulitafutia ufumbuzi suala la mipaka ya eneo hili kwa lengo la kuepusha migogoro hapo baadae.

7. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kujenga vyoo katika eneo hili la kihistoria kwa lengo la kuwaondolea usumbufu wa upatikanaji wa huduma hii muhimu wafanyakazi pamoja na wageni wafikao katika eneo hili.

8. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano kuifanyia matengenezo barabara iendayo katika eneo hili kwa lengo la kuweka mazingira mazuri kwa wageni wanaofika hapo.

**ZIARA KATIKA MRADI WA UKARABATI WA UJENZI WA MAENEO YA KIHISTORIA - PANGO LA WATORO, PANGO LA KIJIJI NA ENEO LA KIHISTORIA CHWAKA TUMBE.**

Kamati kwa mara nyengine tena ilifanya ziara katika miradi hii iliyolenga kukarabati maeneo ya kihistoria kwa lengo la kurudisha haiba na kuilinda historia ya maeneo hayo kwa manufaa ya vizazi vyetu vya sasa na vijavyo. Aidha, Kamati inatoa pongezi zake za dhati kwa hatua za ukarabati zilizofikiwa kwa baadhi ya maeneo hayo.

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

Kamati ilibaini changamoto kadhaa ambazo kuendelea kwake kutakujaigharimu sana Serikali hapo baadae. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:

1. Upungufu mkubwa wa wafanyakazi katika maeneo haya ya kihistoria ni changamoto mtambuka ambayo athari zake ni kubwa katika kuyalinda na kuyahifadhi maeneo haya. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati Wizara imeshachukuwa hatua za kuomba wafanyakazi hao na jumla ya wafanyakazi 145 waliombwa kupitia wizara husika lakini ni ajira 7 tu ndizo zilizotolewa. Unguja nafasi nne na Pemba nafasi 3.
2. Changamoto nyengine ambayo Kamati iliibaini ni ile ya kuchelewa kwa Mkandarasi wa ujenzi kuikabidhi miradi hii kwa wakati uliopangwa. Miradi hii ilianza utekelezaji wake katika mwaka wa fedha 2021/2022 na kwa mujibu wa mkataba, ilitakiwa kukabidhiwa rasmi kwa Wizara mwezi Oktoba 2022 lakini cha kusikitisha hadi Kamati inarudi kwa mara ya pili katika miradi hii, bado utekelezaji wake unasuasua.
3. Kamati pia imebaini changamoto ya matumizi ya maeneo ya miradi kwa shughuli za kijamii ikiwa ni pamoja na kilimo. Wananchi bado wanaendelea kuyatumia maeneo haya kwa shughuli za kilimo, mbali ya kwamba Wizara ilishatoa agizo la kusimamisha shughuli hizo katika maeneo hayo.
4. Changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa wakati nalo limeonekana kuwa ndio chanzo kikubwa kilichozorotesha maendeleo ya miradi hii.
5. Kujengwa kwa bikoni ya kusimamia nguzo ndani ya kaburi katika Msikiti Wivu kunaondosha taswira nzuri ya historia ya eneo hilo.
6. Katika eneo la kihistoria Pango la Watoro, barabara iliyojengwa kufikia katika pango hilo haiko rafiki kutokana na tatizo la kukosa hatua za ngazi (steps). Maelezo yaliyotolewa ni kwamba, Mkandarasi alikaidi agizo la Wizara la kujenga hatua hizo.
7. Changamoto ya ulinzi kwa maeneo mengi ya kihistoria inaenedelea

kuripotiwa katika maeneo haya hali inayosababishwa na uhaba mkubwa wa wafanyakazi kulinganisha na wingi wa maeneo yaliyopo.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kutokana na uhaba mkubwa wa wafanyalkzi uliopo na idadi ndogo ya wafanyakazi iliyopatikana, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Utumishi wa Umma kuliangalia kwa jicho la hisia suala hili na kulipatia ufumbuzi wenye manufaa kwa kuwaajiri wafanyakazi zaidi katika sekta hii, ili lengo la Serikali la kuanzishwa kwa maeneo ya kihistoria nchini liweze kufikiwa.
2. Kutokana na ukweli kwamba, miradi hii muda wake wa utekelezaji umeshamalizika, Kamati inaishauri Wizara kuendelea kumsimamia kwa karibu Mkandarasi wa ujenzi wa miradi hii, ili kuhakikisha kuwa miradi inakamilika kwa muda mchache uliobakia.
3. Tukizingatia uvamizi wa maeneo ya kihistoria unaoendelea siku hadi siku, mbali ya maagizo na maelekezo yanayotolewa na Wizara, Kamati inaendelea kuishauri Wizara kuyazuwia maeneo yote ya kihistoria kwa kuyazungushia uzio japo kwa wa senyenge kwa hatua za awali, ili kuyanusuru maeneo na uvamizi huo unaoendelea.
4. Kamati inaishauri Wizara ya fedha na Mipango kuingiza fedha za miradi hii kwa wakati, ili kuiwezesha Wizara kutekeleza malengo na majukumu iliyojipangia ndani ya mwaka wa fedha husika. Kuchelewa kuingia kwa fedha hizi ndani ya Wizara kunapelekea mikataba ya ujenzi kumaliza muda wake wakati miradi husika bado haijakamilika utekelezaji wake.
5. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kumsimamia Mkandarasi wa ujenzi kuhakikisha bikoni aliyoijenga ndani ya kaburi, anaiondosha haraka kwa lengo la kumuenzi kiumbe aliyezikwa katika eneo hilo na kuidumisha historia yake.
6. Kamati inaendelea kuishauri Wizara kuendelea kuwasimamia kwa karibu sana Wakandarasi wanaopewa dhamana ya ujenzi wa miradi, ili kuepuka hasara na usumbufu unaojitokeza wa kurudia rudia ujenzi wa miradi hii.
7. Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua iliyofikia ya kutaka kuishirikisha jamii kikamilifu juu ya suala la ulinzi wa maeneo ya kihistoria na kuishauri Wizara iendelee na mchakato wa kufikia maamuzi hayo.
8. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kuwa na mipango endelevu itakayohakikisha kuwa, miradi iliyomalizika inaleta tija kwa jamii hasa tukizingatia kuwa miradi hiyo ni mingi na imegharimu fedha nyingi katika utekelezaji wake.

9. Kamati pia inatoa pongezi zake za dhati kwa Mkandarasi wa ujenzi katika msikiti choko, kwa kulirudisha jengo lile katika uhalisia wake. Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kumsimamia Mkandarasi wa ujenzi wa miradi hii kuhakikisha kuwa dosari ndogondogo zilizobainika zinafanyiwa marekebisho kabla ya kuikabidhi miradi hii kwa Wizara.

## ZIARA KATIKA ENEO LA KIHISTORIA - RASI MKUMBUU

Kamati kwa mara nyengine tena imepata nafasi ya kufanya ziara katika eneo la kihistoria Rasi Mkumbuu na kupata historia kamili ya eneo hilo ambalo ni kivutio kizuri kwa wageni watakaofika katika eneo hilo.

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

Katika ziara yake hii, Kamati imebaini changamoto zifuatazo:

1. Miundombinu ya barabara iendayo katika Rasi hiyo sio rafiki kwa wageni kuweza kufika kwa urahisi, hali inayoweza kupunguza morali ya wageni na wenyeji kufika katika eneo hilo.
2. Kamati imebaini changamoto kubwa ya maji ya bahari kuivamia Rasi kwa kasi, hali iliyopelekea baadhi ya miji kuzama kabisa na baadhi ya majengo ya kihistoria yaliyopo hivi sasa kuanza kuporomoka na kuanza kupoteza uhalisia wake. Miongoni mwa majengo hayo ni pamoja na msikiti, makaburi ya washirazi, hodhi la kuhifadhia maji na kisima.
3. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati, eneo lililozunguka Rasi Mkumbuu ni kubwa lakini hadi sasa bado halijahifadhiwa. Hii ni changamoto ambayo inaweza kuzua mgogoro mkubwa kati ya wananchi watakaolivamia eneo hili na Wizara ya Utalii.
4. Upatikanaji wa hati Miliki ya eneo hili pia ni changamoto nyengine ambayo kamati iliibaini. Kamati imesikitishwa kwa kubaini kwamba, kwa mara ya pili sasa Kamati inafika katika eneo hili na kushauri upatikanaji wa hati hiyo lakini bado mchakato wa upatikanaji wake haujakamilika.
5. Changamoto nyengine iliyoelezwa mbele ya Kamati ni elimu ndogo iliyo nayo jamii juu ya umuhimu wa maeneo haya ya kihistoria. Kamati ilielezwa kuwa jamii imekuwa ikilalamika juu ya tozo iliyowekwa kwa wageni wa ndani wanaofika katika eneo hili.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Kutokana na umuhimu wa eneo hili kwa taifa letu, Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano kuifanyia matengenezo barabara iendayo katika Rasi hiyo ili iweze kupitika kwa urahisi na kuweza kuwavutia wageni kuingia kwa wingi katika eneo hilo.
2. Kutokana na umuhimu wa eneo hili, Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kuharakisha mchakato wa ujenzi wa ukuta wenye lengo la kuzuia mmong'onyoko wa ardhi katika eneo hili, lengo ni kuvitunza vivutio viliomo katika eneo hili muhimu kwa wageni toka nje na ndani ya nchi.
3. Ili kulizuia eneo la Rasi kuvamiwa na wananchi pamoja na kuzuia migogoro kati ya wananchi hao na Serikali, Kamati inaishauri Wizara kulihifadhi eneo lote lililozunguka Rasi hii kwa kulijengea uzio japo wa senyenge kwa hatua za awali.
4. Kamati inaendelea kuisisitiza Wizara, kutilia umuhimu utafutaji wa hati miliki kwa eneo hili la kihistoria, kwani hati hii ni nyenzo muhimu katika kulilinda na kulihifadhi eneo hili kama ni urithi kwa vizazi viliopo na vijavyo.
5. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kuziangalia upya tozo zilizowekwa kwa wageni wa ndani, kuhakikisha kuwa zipo rafiki kwao. Sambamba na kuendelea kutoa elimu kwa jamii hiyo juu ya umuhimu wa kutoa tozo hizo kwa maendeleo ya Taifa letu.
6. Kamati inaipongeza Wizara ya Utalii kwa maamuzi yake ya kuandika Andiko la Mradi lenye lengo la kulifanyia maboresho eneo lote la Rasi. Kupitia hali hii, Kamati inaishauri Wizara kuharakisha mchakato wa uanzaji wa mradi huu hasa tukizingatia bajeti yake iko mwishoni kukamilika. (Bajeti ya 22/23).
7. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuendelea kufanya tafiti zaidi juu ya Miji iliyotoweka kwa kuzama kabisa ndani ya eneo hili, kwa lengo la kuweka kumbukumbu iliyo sahihi zaidi ya eneo hili, kama ni urithi mwema kwa vizazi vyetu vya sasa na vijavyo.

## ZIARA KATIKA MAKUMBUSHO YA KASRI YA KIBWENI

Kasri la Kibweni hapo awali lilikuwa likitumika kama ni Ikulu ndogo. Lilijengwa mwaka 1915 na kwa sasa Serikali imelitumia jengo hili kama ni moja miongoni mwa vivutio vya utalii nchini kwa lengo lilelile la kuongeza mapato ya nchi kupitia wageni wanaofika kituoni hapo.

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

Kamati katika ziara yake hii ilibaini changamoto kadhaa kama zifuatazo.

1. Kamati ilibaini changamoto kubwa ya maji ya bahari yanavyoathiri ukuta uliozunguka jengo hili. Kamati ilibaini kuwa uharibifu huu unatokana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa yanayoendelea kuiathiri dunia hivi sasa.

2. Idadi ndogo ya watalii wanaoingia kituoni hapa ni changamoto nyengine ambayo Kamati imeibaini.

3. Kamati pia ilielezwa changamoto ya uhaba wa wafanyakazi kituoni hapo. Hadi Kamati inafika katika kituo hiki, jumla ya wafanyakazi kumi tu ndio waliopo ambao kiuhalisia hawatoshi katika kutekeleza majukumu ya kila siku.

4. Kamati ilielezwa kuwa historia ya kituo hiki bado haijawekwa katika maandiko yaliyo rasmi, maandiko ambayo hadi sasa yapo katika vipeperushi (Bronchures), hali hii inaweza kupelekea kupotea kwa historia yetu ambayo ni urithi mwema kwa vizazi viijavyo.

5. Kamati pia imebaini uwepo wa vianzio vyengine vya mapato katika kituo hiki. Kituo kinamiliki viwanja ambavyo jamii inaweza kuvitumia katika shughuli mbalimbali za kijamii. Utekelezaji wake utaweza kuingiza pato kwa Serikali yetu.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kutokana na umuhimu wa ukuta uliojengwa kuzunguka Kasri hili, ambao kwa sasa unaonekana kuathiriwa na maji chumvi, Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kuchukuwa hatua za haraka za kuirekebisha hali hii kwa lengo la kuzuia uharibifu zaidi usiendelee.

2. Katika kufikia lengo la Serikali la kuongeza idadi ya Watalii wanaoingia nchini

kupitia vituo vyake viliopo, Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kutumia vyombo mbali mbali vya habari kuendelea kukitangaza kituo hiki kwa jamii ili kutoa uelewa zaidi.

3. Kutokana na uhaba wa wafanyakazi uliopo katika eneo hili, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kuajiri wafanyakzi katika sekta hii ili waweze kuziba pengo liliopo hivi sasa ambalo linaweza kuzorotesha maendeleo ya Utalii nchini.

4. Kutokana na umuhimu wa kuitunza historia ya maeneo yetu kwa vizazi vya sasa na vijavyo, Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kupitia Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale kuhifadhi historia ya maeneo haya katika maandiko rasmi kwa lengo la kuepusha upotevu wa historia halisi ya maeneo hayo.

5. Kamati inaishauri Wizara kuvitangaza vianzio vya mapato vilivyomo ndani ya kituo hiki, ili jamii ipate uelewa na iweze kuvitumia na wakati huo huo Serikali kupitia Wizara ya Utalii iweze kujiingizia kipato kupitia vianzio hivyo.

## ZIARA KATIKA KASRI LA SELME – BUBUBU (UNGUJA).

Ni moja miongoni mwa maeneo ya kihistoria ambapo Kamati ilielezwa kuwa historia ya eneo hili, imeungana na historia ya eneo la Bungi kwa Bihole.

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

1. Kamati imebaini changamoto ya kwamba, hadi sasa eneo hili bado halijatangazwa kuwa ni eneo la kihistoria, ambapo kwa sasa eneo hili linamilikiwa na watu binafsi, hali inayoinyima wizara ya Utalii fursa ya kuingiza mapato kupitia eneo hili.
2. Kasri la Selme ni kivutio kizuri cha Utalii kutokana na historia yake pamoja na hali halisi ya Kasri lilipo.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuharakisha mchakato wa kulitangaza eneo hili kuwa ni miongoni mwa maeneo ya kihistoria nchini, hali itakayotoa fursa kwa wageni kutoka ndani na nje ya nchi kuweza kufika katika eneo hilo.
2. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kukaa pamoja na wamiliki wa Kasri hili kwa lengo la kufanya nao mazungumzo ya kuona ni kwa jinsi gani wataweza kuliingiza Kasri hili katika mikono ya Serikali kwa lengo la kuongeza idadi ya vivutio nchini, vitakavyoweza kuingiza pato lake kupitia Utalii.

## ZIARA KATIKA ENEO LA KIHISTORIA MANGAPWANI

Ni moja kati ya maeneo ya kihistoria yaliyo chini ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ambayo yanachukuwa nafasi ya vivutio vikongwe vya Utalii nchini.

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

Kamati katika ziara yake hii ilibaini changamoto zifuatazo:

1. Miundombinu ya barabara za kuingia katika eneo hili si rafiki sana hasa tukizngatia umuhimu wa maeneo haya.

2. Kamati imebaini kuwa Wizara bado haijatoa umuhimu wa kuyaendeleza maeneo haya pamoja na kuwa ni makongwe kihistoria. Maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati yalibainisha kuwa Maeneo haya yaliibuliwa tokea mwaka 1942 lakini cha kusikitisha ni kwamba hadi leo bado yako nyuma kimaendeleo.

3. Kamati pia imebaini kuwa historia ya maeneo haya bado hadi sasa haijahifadhiwa katika maandishi. Kwa mujibu wa maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati yalibainisha kuwa, historia ya maeneo haya imo vichwani mwa watendaji, jambo ambalo ni hatari sana kwani watendaji hawa wengi wao wako mwishoni mwa utumishi wao.

4. Uhaba wa wafanyakazi ni changamoto nyengine ambayo Kamati iliibaini ambapo hadi kamati inapokea taarifa hii ni wafanyakazi watano tu ndio waliopo katika maeneo haya.

5. Uzio katika maeneo haya ya kihistoria bado ni changamoto. Pamoja na kuwa maeneo haya ni ya muda mrefu hadi Kamati inafika katika maeneo haya Wizara ya Utalii bado hijaweka uzio kwa lengo la kuyahifdhi maeneo haya muhimu kwa maendeleo ya taifa letu.

6. Suala la ulinzi katika maeneo haya ya kihistoria pia ni changamoto ambapo Kamati ilibaini kuwa, Wizara imeweka ulinzi ambao haukidhi mahitaji ya maeneo haya, ulinzi ambao unaonekena ni kwa muda wa mchana tu. Hali hii inaweza kutoa fursa kwa wananchi kuingia katika maeneo haya na kufanya uharibifu.

7. Maji ya mvua yanayochanganika na maji chumvi katika pango liliopo katika maeneo haya ya kihistoria ni changamoto ambayo inaweza kuathiri uasili wa kivutio hiki na kupoteza uhalisia wa taarifa zinazotolewa kwa wageni wanaofika katika maeneo haya.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Wizara ya Utalii ishirikiane na Wizara ya Miundombinu kuifanyia matengenezo barabara inayoingilia katika maeneo haya ya kihistoria kwa lengo la kuwarahisishia wageni wanaotaka kufika katika maeneo haya.
2. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kupitia Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale kuyaendeleza na kuyaweka katika muonekano mzuri maeneo haya ili wageni waweze kuvutika nayo na Serikali iweze kuingiza pato lake pale wageni hao watakapofika kutembelea katika maeneo hayo.
3. Kamati inaendelea kusisitiza suala la kuihifadhi historia ya maeneo yetu yote

likiwemo hili la Mangapwani katika maandiko rasmi kwa lengo la kuepusha upotevu na kuweka kumbukumbu nzuri kwa vizazi vyetu vya sasa na vijavyo.

4. Aidha Kamati inaendelea tena kuishauri serikali kupitia Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuajiri wafanyakazi wa kutosha katika taasisi hii ambao wataweza kusaidia katika hatua ya kuutangaza vyema utalii ndani na nje ya nchi.

5. Kutokana na umuhimu wa eneo hili, Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuharakisha ujenzi wa uzio kwa eneo hili ili kulinusuru na uvamizi wa wananchi ambao uzoefu unaonesha kuwa, wananchi wanaoishi karibu na maeneo haya, huyavamia maeneo kwa shughuli za kijamii ikiwa ni pamoja na kilimo.

6. Katika kuhakikisha kuwa, maeneo haya yanabaki salama muda wote, Kamati inaishauri Wizara kupitia Idara ya Makumbusho na Mambo ya Kale kuimarisha ulinzi katika maeneo hayo. Idara ihakikishe kuwa, walinzi wanakuwepo kituoni hapo muda wote hili litasaidia kupunguza uharibifu unaweza kufanywa katika maeneo hayo.

7. Katika kuhakikisha kuwa taarifa zinazotolewa kituoni hapo ni sahihi Wizara ni vyema ikachukuwa hatua za makusudi katika kuhakikisha kuwa, maji ya mvua hayachanganiki na maji chumvi katika kivutio cha asili kiliopo katika eneo hilo.

8. Pamoja na hali hiyo Kamati inatoa pongezi zake za dhati kwa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kwa kulifanyia kazi agizo la Serikali la kutumia mfumo wa kielektroniki katika kukusanya mapato kwa wageni wanaofika katika maeneo haya, hii ni hatua kubwa ya mafanikio ambayo itaweza kuzuia uvujaji na upotevu wa mapato ya Serikali hali itakayosaidia sana katika kupeleka mbele gurudumu la maendeleo nchini.

## ZIARA KATIKA MAENEO YA KIHISTORIA YA KIMAUMBILE

Kamati ilipata fursa ya kuyatembelea maeneo ya kihistoria ya kimaumbile ikiwa ni pamoja na Panga Samaki, Pango Ulingo, Majabali ya Kachunge na Katenga, Mbuyu wa Vasgodagama, Kisiwa ndege na Mto Furaha. Maeneo haya yote yanachukuwa nafasi ya vivutio vipya vya utalii Kisiwani Pemba, ambavyo endapo vitaimarishwa vinaweza kuingiza pato kwa taifa letu na ni urithi mwema kwa vizazi vijavyo.

## ZIARA KATIKA MAENEO YA PANGA SAMAKI, PANGO ULINGO, MAJABALI YA KACHUNGE NA KATENGA NA MBUYU WA VASCODAGAMA.

Kamati ilipofanya ziara katika maeneo hayo ilibaini changamoto zifuatazo: -

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA MAENEO HAYO

1. Barabara za kuingia katika maeneo haya haziko katika hali ya kuridhisha hasa tukizingatia umuhimu wa maeneo haya.

2. Kukosekana kwa uzio katika maeneo haya ni changamoto nyengine inayoweza kuathiri nia njema ya Wzara hii pale wananchi watakapoyavamia maeneo haya kwa shughuli zao za kijamii ikiwemo kilimo. Mfano mzuri ni eneo la Pango Samaki, sote ni mashahidi kwamba karibu na eneo hili wananchi tayari wanajishughulisha shughuli za kilimo na uchimbaji wa kokoto.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inachukuwa nafasi hii kuishauri Serikali kupitia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Mawasiliano kuona ni kwa jinsi gani wanaweza kuzifanyia matengenezo barabara zote ziendazo katika vivutio vipya vya Utalii nchini kwa lengo la kuweka mazingira mazuri yatakayorahisha wageni wa nje na wa ndani kufika katika maeneo hayo kwa wepesi kabisa.

2. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuyapima na kuyahifadhi maeneo haya kwa kuyajengea uzio kwa lengo la kuyanusuru na uharibifu na uvamizi unaoweza kufanywa na wananchi wanaoishi karibu na maeneo hayo.

3. Kutokana na upya wake maeneo haya, Kamati inaendelea kuishauri Wizara ya Utalii kufanya utafiti wa kina kuhusiana na maeneo haya kwa lengo la kupata taarifa sahihi zaidi zitakazosaidia katika uwekaji mzuri wa kumbukumbu kwa wageni watakaofika katika maeneo haya.

4. Pamoja na yote hayo, Kamati inatoa pongezi zake za dhati kwa Wizara ya Utalii

na Mambo ya Kale kwa juhudi kubwa ilizozichukuwa katika kuibua vivutio hivi muhimu kwa maendeleo ya sekta ya Utalii nchini. Aidha Wizara iongeze kasi ya kuibua vivutio vingi zaidi kwa lengo la kuongeza idadi ya watalii nchini pamoja na kutoa elimu kwa jamii kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwa ni njia moja wapo ya kuvitangaza vivutio hivi.

## ZIARA KATIKA KISIWA CHA NDEGE

Ni miongoni mwa kivutio kipya cha Utalii kisiwani Pemba ambacho kimejaaliwa neema ya aina tofauti za ndege.

Kamati katika ziara yake hii imebaini changamoto zifuatazo:

1. Eneo hadi sasa bado halijapimwa na kuweza kujulikana ukubwa wake.
2. Miundombinu ya kufikia katika kivutio hiki bado si rafiki kwa wageni kuweza kufika kwa urahisi.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kushirikiana na Wizara ya Ardhi kulipima eneo hili kwa lengo la kufahamu ukubwa wake na kuweza kulidhibiti.
2. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kuifanyia matengenezo miundombinu iendayo katika kivutio hiki, ili iweze kupitika na kufikika kwa urahisi.
3. Kamati pia inatoa ushauri kwa Wizara ya Utalii kukaa pamoja na wananchi wote wanaofanya shughuli zao katika kisiwa hiki ili kufanya mazungumzo nao juu ya lengo la Serikali la kutaka kuekeza katika eneo hili.
4. Hata hivyo, Kamati inaipongeza Wizara kwa hatua ilizozichukuwa za kubaini kivutio hiki muhimu. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kuendelea na hatua za kukiimarisha kivutio hiki kwa lengo la kuutangaza Utalii kisiwani Pemba na kuongeza pato la Taifa.
5. Kamati pia inaipongeza Wizara ya Utalii kwa mashirikiano yake mazuri iliyonayo na jamii yaliyosaidia kuvumbuliwa kwa kivutio hiki. Hata hivyo Wizara iendelee kutoa elimu ya kutosha kwa jamii juu ya umuhimu wa vivutio hivi nchini hasa tukizingatia kwamba, utalii kisiwani Pemba muamko wake bado ni mdogo.
6. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kuendelea na kasi ya kuvivumbua na kuvitangaza vivutio vipya nchini kupitia vyombo mbalimbali vya habari kwa lengo

la kutoa uwelewa kwa wageni wa ndani na nje ya nchi juu ya uwepo wake.

## ZIARA KATIKA JAMATI LA WAHINDI, MSIKITI PAMOJA NA MAKABURI YA MABOHORA- KENGEJA NA CHAKECHAKE PEMBA.

Ni vivutio vyengine vipya vya utalii vilivyoibuliwa kisiwani Pemba, ambavyo muendelezo wake kutaiwezesha Serikali kuingiza pato litokanalo na Utalii nchini.

### CHANGANOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

1. Eneo lililozunguka Jamati, Msikiti pamoja na Makaburi- Kengeja linaonekana kuwa wazi hali inayowapa fursa wananchi waliolizunguka eneo hili kuingia ndani na kufanya uharibifu. Jamati na Msikiti unaonekana kuvamiwa na kuibiwa baadhi ya rasilimali ziliomo.
2. Ukuta uliozunguka msikiti wa Mabohora Chakechake tayari umeporomoka, hali inayoondosha haiba nzuri iliyokuwepo awali katika eneo hilo na kutoa mwanya kwa wananchi kuingia katika eneo hilo bila ya kizuizi.

### MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kukaa pamoja na wanafamilia wa maeneo haya kwa lengo la kuona ni kwa jinsi gani wataweza kuyafanyia ukarabati majengo ya msikiti, Jamati na Makaburi, kwa lengo la kuyaendeleza na kuyahifadhi kwa manufaa yao na taifa kwa ujumla. Maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati yanathibitisha uwepo wa wanafamilia hawa na utayari wao katika kushirikiana na Wizara kwa lengo la kulifanikisha hili.
2. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kukaa pamoja na uongozi wa msikiti wa Mabohora Chakechake kuona ni kwa jinsi gani itakavyoweza kuujenga ukuta uliozunguka msikiti huo. Lengo ni kuzuia uingiaji holela wa watu ndani ya msikiti huo.
3. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kuishirikisha kikamilifu jamii iliyozunguka maeneo ya Jamati, misikiti na makaburi, kufanya hivyo kutasaidia sana katika utatuzi wa changamoto ndogondogo pale zinapotokezea ikiwa ni pamoja na ulinzi.

## ZIARA KATIKA GATI YA ZAMANI

Gati hii imejengwa na Waingereza katika karne ya kumi na tisa, ikiwa ni kivutio kingine

kizuri cha Utalii kisiwani Pemba.

## CHANGAMOTO ZILZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

1. Kamati imebaini changamoto kubwa ya athari ya maji chumvi dhidi ya gati hii. Maji ya bahari yameanza kuiporomoa gati hii hali inayohatarisha usalama wa watumiaji na uwepo wa gati yeneyewe.
2. Changamoto nyengine iliyobainika ni ile ya Mnara uliopo katika gati hiyo kuwa hatarini kuanguka kutokana na athari za maji ya bahari.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kukiingiza kivutio hiki katika miradi ya maendeleo ya Wizara kwa lengo la kuharakisha ukarabati wake.
2. Kamati inaishauri Wizara kuchukuwa hatua za dharura katika kuuhami Mnara huo ili historia ya eneo lile iweze kubakia na kuwa urithi mwema kwa wageni na vizazi vyetu vya sasa na baadae.
3. Kamati pia inaishauri Wizara ya Utalii kufanya tafiti zaidi ili kubaini uwezekano wa kuunganisha gati hii toka sehemu moja na nyengine kwa kuruhusu shughuli za utalii wa majini ziweze kuimarika zaidi kwa kutumia boti ndogondogo kutoka gati ilipo kwenda sehemu nyengimne kama Mithali.

## ZIARA KATIKA MTO FURAHA

Kamati ilipata nafasi ya kufanya ziara katika kivutio cha Utalii -Mto Furaha kilichopo Vitongoji Kisiwani Pemba, ambapo kwa sasa mto huu unatumiwa na wanajamii kwa shughuli za uvuvi. Kivutio hiki kimevumbuliwa na wanajamii ambao kwa umoja wao waliweza kuunda Jumuiya yao iliyojulikana kwa jina la ***Pemba Swimming Sports and Marine Center*** yenye lengo la kutoa uelewa kwa jamii nzima kisiwani Pemba juu ya uwepo wa mto huu na umuhimu wake kitaifa na kimataifa.

## CHANGAMOTO ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA HII

Katika ziara yake hii, Kamati ilibaini changamoto zifuatazo:

1. Kamati ilibaini mto huu ni kivutio kizuri cha Utalii lakini mazingira yake si rafiki kwa wageni kuweza kufika na kukitumia kivutio hiki.
2. Kuingia na kutoka kwa maji katika mto huu ni changaomto nyengine ambayo

Kamati iliibaini. Changamoto hii inaweza kuathiri sana uingiaji wa wageni katika kivutio hiki, kutokana na kuwepo kwa uwezekano wa wageni hao kukaa na kusubiria maji ili waweze kusafiri kuelekea ng'ambo ya pili.

## MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuyaboresha mazingira yaliyozunguka mto huu kwa lengo la kuwavutia wageni kupata hamu ya kuyatembelea maeneo haya.
2. Kutokana na hali iliyopo hivi sasa ya uingiaji wa maji katika mto huu, Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kwa kushirikiana na Jumuiya hii, kufanya utafiti wa kina juu ya nyakati za uingiaji na utokaji wa maji katika mto huu, ili kuwaepushia usumbufu wageni watakaofika katika eneo hili, wa kusubiria maji kwa muda mrefu kama Kamati ilivyobaini.
3. Kamati inaipongeza sana Jumuiya hii kwa kujitoa kwake na kukubali kushirikiana na Wizara ya Utalii kwa kuandika Andiko la Mradi ambalo lina lengo la kuinyanyua sekta ya Utalii nchini.
4. Kamati inaishauri Wizara ya Utalii kutoa ushirikiano wa hali na mali kwa Jumuiya hii ili kuhakikisha eneo hili linaboreshwa na kuimarishwa na mwisho wa siku tuone kuwa shughuli za Utalii zinaanza kikamilifu katika eneo hili. Kamati inaamini kuwa kuanza kwa shughuli za kitalii katika eneo hili kutasaidia sana katika kuutangaza utalii nchini.
5. Kamati inaishauri Wizara suala la kutoa Elimu liwe endelevu hasa kwavile wananchi wanaonekana kua na muamko juu ya shughuli za utalii.

## PROGRAMU KUU YA UTANGAZAJI NA UHAMASISHAJI WA UTALII

Programu hii imelenga kuongeza uelewa kwa wakaazi wa Tanzania na jamii ya kimataifa kuhusiana na bidhaa na huduma za utalii zilizopo Zanzibar.

Progamu hii inatekelezwa na Kamisheni ya Utalii kupitia Idara ya Masoko yenye jukumu la kupanga mikakati na kuitangaza Zanzibar kiutalii ndani na nje ya nchi.

## KAMISHENI YA UTALII

Kamisheni ya Utalii imeundwa kwa Sheria namba 9 ya mwaka 1996 ambayo ilifutwa kwa Sheria namba 6 ya mwaka 2009. Kwa sasa Kamisheni ya Utalii inaendeshwa kwa kufuata Sheria No.6 ya mwaka 2009 kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria Na.7 ya mwaka 2012.

## MAFANIKIO YA KAMISHENI YA UTALII

Kamisheni imefanikiwa kutekeleza yafuatayo: -

1. Kupitia Kamisheni ya Utalii Wizara ya Utalii imefanikiwa kuandaa na kushiriki maonesho, mikutano na makongamano ya Utalii ya kitaifa na kimataifa ili kuvutia wageni kuweza kuvitembelea vivutio vya Utalii vya Zanzibar.

2. Kupitia Kamisheni ya Utalii imefanikiwa kuwaalika waandishi wa habari za utalii wa kimataifa, wamiliki wa mitandao ya kijamii na watu mashuhuri ili Zanzibar ipate fursa ya kutangazwa kupitia watu hawa kwa gharama nafuu.

3. Kamisheni imefanikiwa kuandaa na kutoa matangazo ya utalii katika majarida, televisheni za kitaifa na kimataifa na mabango ya kiektroniki ili kuwavutia watalii wengi zaidi kutoka katika masoko ya asili na mapya.

## CHANGAMOTO ZA KAMISHENI YA UTALII - PEMBA

1. Kamati ilielezwa kuwa idadi ndogo ya watalii wanaoingia kisiwani Pemba kuwa ni miongoni mwa changamoto kubwa ambapo idadi hiyo inayopelekea kushuka kwa pato la taifa.

2. Uhaba wa fedha wa kuendeshea kazi za Kamisheni, hali hii inatokana na ufinyu wa bajeti ambayo inakwamisha utekelezaji wa kazi za Kamisheni.

3. Kamati ilibaini uhaba mkubwa wa wafanyakazi uliopo katika taasisi hii kisiwani Pemba. Kamati ilisikitishwa na takwimu halisi ya wafanyakazi iliyopo kwa sasa ambapo Kamati iliarifiwa kuwa Ofisi hii ina jumla ya wafanyakazi 18 tu hali inayoleta ugumu katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku hasa tukizingatia unyeti wa taasisi na majukumu yake.

4. Changamoto nyengine ambayo Kamati iliibaini ni ukosefu wa ofisi ya Kamisheni kwa Pemba. Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa mbele ya Kamati ni kwamba kwa sasa Kamisheni imekodi jengo la mtu binafsi kwa gharama ya

shilingi 600,000/= kwa mwezi ambayo ni sawa na shilingi 7,200,000/= kwa mwaka.

5. Aidha, uhaba wa fedha za bajeti unaoingizwa katika Taasisi hii ni changamoto nyengine ambayo inarudisha nyuma kasi ya utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa. Kamati inaishauri serikali kupitia Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuiongeza bajeti ya Kamisheni kwa lengo la kuiwezesha kuutangaza Utalii ndani na nje ya nchi.

6. Utegemezi wa OC kwa Kamisheni katika kutekeleza majukumu yake inaonekena kuwa ni changanoto nyengine inayozorotesha utekelezaji wa majukumu ya taasisi hii siku hadi siku.

MAONI, MAAGIZO NA USHAURI WA KAMATI

1. Kamati inaishauri Serikali kupitia Kamisheni ya Utalii kuharakisha zoezi la kuweka vivutio vya Utalii kisiwani Pemba kwa lengo la kuimarisha utalii na kuongeza kasi ya maendeleo katika kisiwa hiki kama agizo la Mheshimiwa Rais alivyolitoa katika hotuba zake.

2. Kamati inaishauri Serikali kuiongezea bajeti ya kutosha Kamisheni ya Utalii kwa lengo la kuiwezesha Kamisheni kuweza kutekeleza majukumu yake ya kuutangaza utalii nje na ndani ya nchi.

3. Kamati inaishauri Serikali kuajiri wafanyakazi wa kutosha kwa ajili ya Taasisi hii muhimu kwa maendeleo ya Wizara yetu kisiwani Pemba. Idadi ndogo ya wafanyakzi iliyopo hivi sasa imekuwa ni kikwazo kikubwa cha kuleta ufanisi ndani ya taasisi yetu hii.

4. Kamati inaishauri Serikali kujenga majengo bora na ya kisasa kwa ajili ya ofisi ya Kamisheni kisiwani Pemba kwa lengo la kuepusha usumbufu na gharama kubwa inayotumika katika kulipia kodi kwa majengo ya watu binafsi. Kuendelea kwa hali hii kutaendelea kuitia Serikali gharama kubwa, ambapo gharama hiyo ingeweza kutumika katika mambo mengine ya kuiletea maendeleo taifa letu.

5. Kamati inaishauri Serikali juu ya fedha inayokusanywa na Kamisheni, kwamba ibakie

asilimia ndogo ibakie ndani ya taasisi hii kwa lengo la kuiwezesha kujikimu katika kutekeleza majukumu yake kwa urahisi na kwa ufanisi zaidi na pia waache kutegemea OC pekee ambayo ni dhahiri kwamba uingiaji wake hauko vizuri.

**PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YA UTALII**

Programu hii ina jukumu la kusimamia na Kuratibu Mipango Mikuu, Sera na Tafiti pamoja na Usimamizi na Uendeshaji mzuri wa Rasiliamali watu katika Wizara

Programu hii inajumuisha programu ndogo zifuatazo: -

i) Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji katika sekta ya Utalii na Mambo ya Kale;

ii) Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamai Mipango Mikuu ya Wizara;

iii) Programu ndogo ya Kuratibu na Kusimamia Utawala, Uendeshaji na Mipango ya Ofisi Kuu Pemba.

**ZIARA ZA KAMATI KUANGALIA MAENDELEO YA PROGRAMU HII.**

Kamati katika kazi zake ilifanya ziara katika maeneo mbali mbali pamoja na kukagua Miradi ya maendeleo kwa lengo la kutathmini maendeleo yake pamoja na tija iliyopatikana. Kupitia program ndogo hizi Kamati ilifanya ziara katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:

i) Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba;

**ZIARA KATIKA OFISI YA AFISA MDHAMINI - PEMBA**

Kamati ilipata nafasi ya kufanya ziara katika ofisi ya Afisa Mdhamini na kupatiwa taarifa juu ya uendeshaji wa taasisi na Idara mbali zilizo chini ya Ofisi hii.

**CHANGAMOTO ZIARA KATIKA OFISI YA AFISA MDHAMINI – PEMBA**

1. Kamati ilielezwa changamoto ya uhaba wa wafanyakazi unaozikabili taasisi na Idara zilizomo katika Wizara hii ya Utalii na Mambo ya Kale. Kamati imesikitishwa na taarifa iliyotolewa mbele ya Kamati kwamba, Wizara ya Utalii kwa upande wa Pemba haina Afisa Sheria, jambo ambalo halikubaliki kwa

sababu kukosekana kwa mwanasheria ndani ya Wizara huwaletea usumbufu mkubwa pale zinapotokea changamoto zinazohitaji utatuzi wa kisheria. Aidha, Kamati inaamini kuwa upungufu mkubwa wa wafanyakazi uliopo hivi sasa katika Wizara hii kunaweza kupunguza kasi ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ndani ya taasisi na Idara zake. Sote ni mashahidi juu ya ukweli kwamba Wizara hii ni moja miongoni mwa Wizara nyeti inayochangia kwa kiasi kikubwa pato la taifa la nchi yetu litokanalo na uingiaji wa wageni toka nje.

2. Changamoto nyengine ambayo ilielezwa mbele ya Kamati ni ufinyu wa bajeti inayopangwa na uingiaji mdogo wa OC kwa idara na taasisi ziliopo kiswani Pemba, hali inayopelekea baadhi ya majukumu kushindwa kutekelezwa kama yalivyopangwa.

3. Uhaba wa vitendea kazi ikiwemo vyombo vya usafiri imeelezwa kuwa ni miongoni mwa changamoto inayozikabili Taasisi na Idara ziliomo katika Wizara hii. Kamati ilifahamishwa kuwa vitendea kazi hivyo viliopo ikiwemo magari ni machache na yaliyochakaa sana hali inayokwamisha utekelezaji wa kazi za taasisi ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji katika maeneo ya kihistoria yaliopo kisiwani Pemba ambapo inafahamika kwamba maeneo mengi yapo katika masafa ya mbali ambayo inawawia vigumu wafanyakazi hao kuyafikia kwa urahisi.

4. Changamoto nyengine ambayo ilibainika ni ufinyu wa ofisi zinazotumiwa na taasisi na Idara za Wizara hii kisiwani Pemba. Kamati ilishuhudia ofisi zinazotumiwa na Taasisi na Idara hizi si rafiki kwa matumizi ya ofisi hali inayoweza hata kuhatarisha afya za wafanyakazi wetu.

5. Uchakavu wa maeneo ya kihistoria nayo imebainika kuwa ni miongoni mwa Changamoto moja wapo iliyopo kwa sasa. Maeneo mengi ya kihistoria yanaonekana kupoteza haiba na uhalisia wake kutokana na uchakavu huo, hali inayoweza kupunguza idadi ya wageni wetu kuja kuyatembelea maeneo hayo.

6. Kamati pia ilielezwa changamoto ya uharibifu wa maeneo ya kihistoria. Kamati ilibaini kuwa, uharibifu huu unafanywa na wananchi wanaoishi karibu na maeneo hayo kwa kuyavamia kwa kujenga nyumba za makaazi na hata kufunga wanyama wao.

## MAONI NA USHAURI WA KAMATI

1. Serikali inapaswa kuliangalia kwa jicho la pekee suala la kuongeza idadi ya wafanyakazi katika Wizara hii muhimu kwa lengo la kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake ili Serikali iweze kufikia malengo iliyojipangia ya kuimarisha uchumi wake.

2. Kamati inaishauri Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa Wizara hii na kuingiza OC kwa wakati ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kwa wakati na kwa ufanisi. Hata hivyo Kamati inachukua nafasi hii kuipongeza Wizara kwa kuendelea kutekeleza majukumu yake hayo kwa ufanisi pamoja na mgao mdogo wa fedha wanaopatiwa.

3. Kamati inaishauri Serikali kuipatia Wizara vitendea kazi vya kutosha vikiwemo vyombo vya usafiri kwa lengo la kurahisisha utekelezaji wa majukumu ikiwa ni pamoja na kuyafuatilia maeneo ya kihistoria ambayo mengi yao imeelezwa kuwa yako mbali kufikika.

4. Kamati inaishauri Serikali kujenga majengo mazuri na rafiki kwa ajili ya Idara na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale ili kuondosha kabisa changamoto kubwa ya kukosekana kwa ofisi ambayo inarudisha nyuma kasi ya maendeleo kwa taasisi zetu.

5. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya utalii kuendelea na kasi yake ya kuyaimarisha maeneo ya kihistoria ambayo bado hayajaimarishwa na kuendelezwa kwa lengo la kurudisha haiba nzuri ya majengo hayo na kuyaingiza katika idadi ya vivutio kwa wageni wanaofika kutembelea katika maeneo hayo.

6. Kamati inaiomba Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale kuchukua hatua za haraka za kuirebisha hali iliyopo hivi sasa ya uharibifu wa maeneo ya kihistoria kwa kuyawekea uzio maalumu, kwa lengo la kuzuia uharibifu unaofanywa na wananchi wanaoishi karibu na maeneo hayo usiendelee na kuyaweka maeneo hayo katika muonekano wake wa asili.

## SEHEMU YA TATU

### HITIMISHO

Katika kutekeleza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar, Kanuni za Baraza la Wawakilishi na Sheria nyenginezo, Kamati imetoa maelekezo na ushauri wake ambao tunaamini kuwa utasaidia katika kuleta ufanisi katika kutekeleza majukumu ya Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda na Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale. Maoni na Ushauri uliotolewa na Kamati una lenga kuwawakilisha vyema wananchi wa Zanzibar na kuona kuwa maslahi ya wananchi hao, kwa mujibu wa sheria yanapewa kipaumbele. Kamati yetu inatumai kuwa maelekezo na maoni yote yaliyotolewa na Kamati kwa Wizara hizo yatazingatiwa kwa lengo la kutoa huduma zilizo bora zaidi kwa wananchi wote wa Zanzibar.

Kamati inatoa shukurani zake za pekee kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi, kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake vizuri, lakini zaidi kwa ushauri walioupatia Kamati yetu katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.